SUPA JACKPOT
TZS. 1,069,861,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mwili** Mtanzania aliyefia vitani Ukraine watua, kuagwa leo

UKURASA 3


Ujio mikutano ya vyama, UVCCM tutafanya haya

siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Putin amebakia kuwatumbua makamanda, vita ikimwelemea

SAMIA KUONGOZA AFRIKA DAVOS
**Ni ishara kukubalika kitaifa, kimataifa, maridhiano, usawa kijinsia vyampaisha**

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Januari 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581201

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa

UKATILI KINGONO SHULENI

# Timu ya uchunguzi yawekewa vigingi

• **Wajumbe**, Kamishna wa Elimu wazuiwa kuingia baadhi ya shule binafsi... *Endelea ukurasa 2*



Kazi ya ujenzi wa majengo ya mradi wa stendi mpya ya mabasi Mwenge, ikiendelea katika Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam jana baada ya ujenzi kusimama kwa muda mrefu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## CCM yatangaza kiama viongozi walalamikaji pasi na kufanya kazi

UKURASA 3



## Polisi yaahidi ulinzi mapokezi ya Lissu

UKURASA 2

**MICHEZO** **FEI TOTO AMUUMIZA KICHWA NABI** UK.24

**KATUNI** UK.6



Waombolezaji, ndugu, jamaa na marafiki wakishiriki kumzika marehemu Henry Massawe nyumbani kwake Kiaraka Magengeni, Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani jana. **Habari kamili Uk. 4** **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

# Timu ya uchunguzi yawekewa vigingi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TIMU iliyoundwa na serikali kuchunguza vitendo vya ukatili wa kingono na udhalilishaji wanaofanyiwa baadhi ya wanafunzi nchini imedai kuzuiwa kuingia kwenye baadhi ya shule binafsi kutekeleza majukumu yake.

Shule hizo ambazo hazitajajwa majina, zimedaiwa kuizuia timu hiyo kufanya kazi yake kwa madai kuwa sera za shule hizo haziruhusu watu wa nje kuingia shuleni hapo. Timu hiyo imeanzia Mkoa wa Kilimanjaro kufanya uchunguzi wa suala hilo.

Vilevile, shule hizo zimedai kuwa ni lazima wazazi wa wanafunzi wahusishwe kwanza na waridhie watoto wao kushiriki kwenye uchunguzi huo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, alibainisha hayo wakati wa kikao na Maofisa Elimu Msingi na Sekondari pamoja na wadhibiti ubora wa mkoani Kilimanjaro kilichofanyika mjini hapa juzi.

"Leo (juzi) asubuhi, nimepokea simu kutoka kwa Kamishna wa Elimu akidai kuna taasisi (shule) zimewagomea kufanya uchunguzi, zimewaambia haziwezi kuwaruhusu kuingia shuleni mpaka kila mzazi wa mtoto aliyepo kwenye shule hizo aruhusu mtoto kuhojiwa, huku wakiongeza kuwa sera zao haziruhusu 'watu back' (watu wa nje) kuingia shuleni.

"Hapo ninashangaa 'mtu back' ni nani? Aliyekwenda ni Kamishna wa Elimu mwenyewe, mwenye mamlaka ya kusajili na kutoa vibali vya shule, ndiye anayeitwa 'mtu back'. Hii imetufikirisha sana," Katibu Mkuu alisema.

Timu hiyo iliundwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, baada ya Nipashe kuchapisha habari ya uchunguzi kuhusu wanafunzi kufundishwa kulawitiana shuleni wakiahidiwa kupewa zawadi zilizoambana na ofa ya kupewa nafasi ya kuongea kwa simu na wazazi wao.

Ikumbukwe kuwa taratibu za shuleni nchini zinazuia wanafunzi kutumia simu shuleni na wazazi hawaruhusiwi kuongea kwa simu na watoto wao wanapokuwa shuleni isipokuwa kwa utaratibu maalum kunapokuwa na dharura, na katika hilo simu ya uongozi wa shule hutumika.

Katibu Mkuu allisema wizara imepata shaka kubwa kwa baadhi ya shule, hasa binafsi kwa kitendo cha kuzuia maofisa wa serikali kutekeleza wajibu wao.

"Kusema ni kwa nini wanagomea timu kufanya uchunguzi, siwezi kujua maana wao ndiyo wanajua wenyewe, pia kwa sasa siwezi kuzitaja taasisi (shule) kwa kuwa timu iliyotumwa mkoani Kilimanjaro inaandaa ripoti itakayoonyesha ni shule zipi zilizokataa ili Watanzania wazijue," alisema.

Aliagiza shule zilizosajiliwa nchini na zimepewa vibali vya kufanya kazi ya utoaji wa elimu chini ya sheria, kuacha kuwazuia watendaji wa serikali wanapokwenda kufanya kazi mbalimbali, ukiwamo ukaguzi.

"Endapo taasisi (shule) zitafanya vinginevyo, wizara itafikiria tofauti na hatua kali zitachukuliwa ili kukomesha jambo hilo," Dk. Michael alionya.

Katibu Mkuu alibainisha kuwa timu ya ukaguzi iliyoko mkoani Kilimanjaro, tayari imepita kwenye baadhi ya shule, akielekeza kuwa ni wajibu wa maofisa elimu msingi na sekondari pamoja na wadhibiti ubora kushirikiana na maofisa ustawi wa jamii nyakati za ukaguzi ili wafanye kazi hiyo kwa ufanisi zaidi.

Mkoa wa Kilimanjaro una shule za awali 961 (za serikali 869 na binafsi 92); za msingi 992 (za serikali 872 na binafsi 120) na za sekondari ni 352 (binafsi 127 na za serikali 225, huku 71 zikiwa za kidato cha tano na sita).

Timu hiyo inayopita kuchunguza ukubwa wa tatizo la vitendo vya ukatili wa kingono na udhalilishaji mkoani Kilimanjaro inajumuisha Kamishna wa Elimu, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Elimu na Mwanasheria wa Wizara.

**VITABU TATIZO**

Katibu Mkuu pia aliweka wazi wamepokea taarifa za kuwapo machapisho na vitabu mbalimbali visivyo na maadili, vinatumika kwenye baadhi ya shule nchini.

Alisema wizara imeanza kuzifanyia kazi taarifa hizo ili kumshauri waziri mwenye dhamana hatua za kuchukua.

"Yawezekana kuna mahali serikali ilizembea na baadhi ya machapisho na vitabu visivyo na maadili ya kitanzania vikaingia nchini.

"Ni wakati wa kufanya uchunguzi katika shule na maktaba mbalimbali ili kujionea ukubwa wa tatizo. Kwa mujibu wa sheria, waziri wenye dhamana ana haki na mamlaka ya kupiga marufuku machapisho na vitabu hivyo kutumika shuleni," Katibu Mkuu alihitimisha ufafanuzi wake.

# Polisi kuimarisha ulinzi ujio wa Lissu

**Na Restuta James**

WAKATI macho na masikio ya wafuasi na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), yakielekezwa Dar es Salaam anakowasili Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, Jeshi la Polisi limewahakikishia ulinzi na usalama likieleza 'tumejipanga kuona usalama unaimarika.'

Lissu ambaye aligombea urais kwa tiketi ya CHADEMA mwaka 2020, anawasili nchini akitokea nchini Ubelgiji ambako ameishi kwa takribani miaka minne akifanyiwa matibabu baada ya watu wasiojulikana kumshambulia kwa risasi mwaka 2017.

Akizungumza na NIPASHE jana, Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema askari wake wamejipanga vizuri kuhakikisha kiongozi huyo na wafuasi wake wanaongozwa na kulindwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema, Jeshi la Polisi Kanda Maalum limejipanga kuuongoza msafara wa kiongozi huyo kwa namna ambayo haitaathiri ujenzi wa barabara na ule wa reli ya kisasa unaoendelea barabara ya Nyerere inayotokea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

"Tutampitisha kwenye barabara ambazo ujenzi haundelei kwa sababu ule ni mradi mkubwa wa kitaifa...tutampitisha kwenye barabara ambazo hazitaathiri masuala ya ujenzi," alisema.

Kuhusu usalama, Kamanda Muliro alisema: "Polisi tumejipanga kama kawaida... tutaendelea na shughuli kuona usalama unaimarika."

Alisema jeshi hilo litazingatia mifumo yake kuhakikisha wafuasi, wanachama na viongozi wa chama hicho wanapata ulinzi stahiki.

"Na yeye (Lissu), kama Mtanzania atakuwa sehemu ya Watanzania wengine ambao wanapata usalama huu huu," alisema.

Mwenyekiti wa kamati maalum inayoratibu mapokezi ya Lissu, Peter Msigwa, aliiambia NIPASHE jana kwamba viongozi wote waandamizi wa chama hicho wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, watakuwapo uwanja wa ndege kumpokea.

Alisema kiongozi huyo ambaye atawasili saa 7:30 mchana ataelekea moja kwa moja viwanja vya Bulyaga vilivyoko Temeke mwisho kuhutubia wananchi.

Alisema baada ya mkutano wa leo, chama hicho kitakuwa na vikao vya faragha kwa siku mbili kuanzia kesho jijini Dar es Salaam.

Kamati ya Msigwa iliyopewa jina la 'Lissu Home Coming' imewaomba wafuasi wa chama hicho pamoja na wakazi wa jiji la Dar es Salaam, kujitokeza kwa wingi kumpokea kiongozi wao huyo.

"Niwakaribishe wakazi wa Dar es Salaam tukampokee shujaa wetu uwanja wa ndege na kisha twende Temeke tukamsikilize Lissu maana anafundisha, anaelimisha na tutapata mambo mengi kutoka kwake," alisema Msigwa juzi.

Lissu aliondoka nchini Septemba 7, 2017 kwenda Nairobi, Kenya kwa matibabu baada ya kushambuliwa kwa risasi katika makazi yake 'Area D' jijini Dodoma, muda mchache baada ya kutoka bungeni na hivyo kukimbizwa hospitalini mkoani hapo hata hivyo, ilibidi asafirishwe kwa matibabu zaidi nchini Kenya.

Nairobi alipatiwa matibabu kwa muda mfupi na kusafirishwa hadi nchini Ubelgiji ambako alipatiwa matibabu yote hadi aliporejea nchini Tanzania kwa mara ya kwanza Julai 27, 2020 kwa ajili ya kushiriki uchaguzi mkuu akiwania nafasi ya urais kwa tiketi ya chama chake.

Novemba 10, 2020, Lissu aliondoka kurudi Ubelgiji baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, akidai kwamba usalama wa maisha yake ulikuwa hatarini.

Akitoa salamu za mwaka mpya, Januari 13, mwaka huu, alieleza kusudio lake la kurejea Tanzania Januari 25.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, alisema tayari maandalizi ya kurejea kwa viongozi wote wa chama hicho ambao ni wakimbizi wa kisiasa yanafanyika kwa hatua mbalimbali.

Alitaja viongozi wengine wanaojiandaa kurejea nchini mbali na Lissu, pamoja Godbless Lema ambaye alikuwa mbunge wa Arusha Mjini.

"Na kuhusu viongozi wengine wa chama chetu kurejea nchini akiwamo Lema, wanaendelea kufanya maandalizi na watakapokamilisha taratibu zao watasema wanarejea lini, lakini maandalizi yanaendelea huko waliko na yako hatua mbalimbali, kwa hiyo wakikamilisha, watatoa taarifa rasmi," alisema Mrema hivi karibuni katika mkutano na waandishi wa habari.

# Mwili wa Mtanzania aliyefariki vitani Ukraine wawasili, serikali yatoa onyo

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI maalumu inayoratibu mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, iliyopewa jina la 'Lissu Home Coming', imewaomba wafuasi wa chama hicho na wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi kesho kumpokea kiongozi huyo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mch. Peter Msigwa, Lissu atawasili kesho saa 7:30 mchana kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere(JNIA).

Mch. Msigwa alisema kuwa baada ya kuwasili, Lissu atakwenda moja kwa moja kwenye viwanja wa Mwembe Yanga, Temeke kufanya mkutano wa hadhara kuzungumza na Watanzania.

“Mimi ni mwenyekiti wa kamati ndogo inayotokana na Kamati Kuu ya chama, maarufu Lissu Home Coming, na ndio maana niliondoka Mwanza kuja hapa kwa sababu hiyo ya kushughulikia mapokezi yake kwa kushirikiana na CHADEMA Kanda ya Pwani.

“Na baadhi waliopo katika kamati hii ni pamoja na Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Pwani, Baraka Mwago, Grace Kiwelu na mwingine wa Zanzibar. “Kwa hiyo, niwakaribishe wakazi wa Dar es Salaam tukampokee shujaa wetu uwanja wa ndege na kisha twende Temeke tukamsikilize Lissu maana anafundisha, anaelimisha na tutapata mambo mengi kutoka kwake,” Mch. Msigwa alisema.

Lissu aliondoka nchini Septemba 2017 kwenda Nairobi, Kenya kwa matibabu baada ya kushambuliwa kwa risasi kwenye makazi yake Area D jijini Dodoma muda mfupi baada ya kutoka bungeni.

Baada ya shambulio, alikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu na baadaye alisafirishwa kwenda Nairobi, Kenya kwa matibabu kisha kusafirishwa kwenda Ubelgiji ambako aliendelea na matibabu hadi aliporejea nchini kwa mara ya kwanza Julai mwaka 2020, akashiriki Uchaguzi Mkuu akiwania nafasi ya urais kwa tiketi ya CHADEMA.

Novemba 10, 2020, Lissu aliondoka tena nchini, akisindikizwa hadi uwanja wa ndege na Balozi wa Ujerumani kwenda Ubelgiji baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, akidai usalama wa maisha yake ulikuwa shakani.

Januari 13, mwaka huu, Lissu alizungumza na Watanzania kupitia mitandao ya kijamii na kueleza kusudio lake la kurudi nchini Januari 25. Wiki iliyopita, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema maandalizi ya kurejea kwa viongozi wote wa chama hicho ambao ni wakimbizi wa kisiasa, yanafanyika kwa hatua mbalimbali.

Alitaja viongozi wengine wanaojiandaa kurejea nchini mbali na Lissu kuwa ni pamoja na Godbless Lema ambaye alikuwa Mbunge wa Arusha Mjini.

## CCM yatangaza kiama viongozi walalamishi wasiochukua hatua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ametangaza kibano kwa viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri wanaoshindwa kutimiza wajibu wao na kugeuka kuwa walalamikaji.

Amesema chama kitaanza ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani, utendaji wa viongozi, namna wananchi wanavyohudumiwa na kuwashughulikia watakaobainika kutotimiza wajibu wao.

Akizungumza jana kwenye hafla ya mapokezi ya sekretarieti ya CCM Taifa Makao Makuu, Dodoma, Chongolo, alisema chama hicho hakitamchekea mtu aliyepewa dhamana serikalini na kushindwa kutimiza wajibu wake wa kuwatumikia wananchi. “Ukiwa waziri umepewa dhamana ya kusimamia eneo lako wewe ndiyo msimamizi wa kanuni, sheria na zimekupa mamlaka ya kufanya maamuzi na pale inapohitajika kufanyika mawasiliano ya ziada na ya juu yako umepewa dhamana ya kufanya hivyo.”

Alisema baada ya CCM kupewa dhamana liliundwa Baraza la Mawaziri, waliteuliwa wakuu wa mikoa, wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Mikoa, Wakurugenzi hadi watendaji wa vijiji na tatizo lililopo ni baadhi kutojua dhamana walizopewa.

“Sasa hivi kumeibuka tabia ya kiongozi anapewa eneo naye analalamika, unamkuta waziri badala ya kufanya maamuzi ili mambo yatokee yeye anabaki analalamika, Katibu Mkuu anapewa wizara badala ya kutimiza majukumu yake anabaki analalamika...hatupo kwenye wakati wa kusubiri malalamiko ya watu waliopewa dhamana,” alionya. Chongolo alisema wapo kwenye wakati wa kutenda na kuwataka viongozi hao watambue wana dhamana wamepewa eneo la kulitumikia.

Alisema Watanzania wanataka huduma, barabara, maji, elimu na miundombinu mizuri, hawataki maneno.

Kadhalika, alisema wakiwaona watu wanapata neno la kuwanyoshea kidole watambue kuwa hawajakaa sawa sawa na hawatimizi wajibu wao.

“Niwaambie mimi naitwa Chongolo lakini nikiwa Katibu Mkuu ni Katibu Mkuu, hatutacheka na mtu yeyote tunachotaka ni kuona tija na matokeo ya kile tulichopanga,” alisema.

Aidha, alishukuru kwa kuaminiwa kuendelea kutumikia nafasi hiyo na kuahidi kuendelea kuhakikisha dhamira ya CCM inatimia.

Awali, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Alhaj Adam Kimbisa, alisema CCM inampongeza Chongolo kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena kuwa Katibu Mkuu wa CCM.


## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together, we can build a better life)

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2022.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2022 | Robo Mwaka iliopita 30 Septemba 2022 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 595.79 | 1,035.91 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 4,942.86 | 5,700.62 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 43,769.98 | 43,397.06 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 504.40 | 1,872.40 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 0.04 | 44.68 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,179.14 | 5,333.24 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 50,045.03 | 47,624.19 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,152.49 | 1,499.65 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 429.07 | 532.62 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **105,618.80** | **107,040.38** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 9,984.60 | 11,595.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 53,334.13 | 52,432.17 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,651.62 | 1,551.67 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 245.58 | 620.20 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **65,215.93** | **66,199.04** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29*** | **40,402.87** | **40,841.33** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 308.15 | 1,367.28 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 6,608.27 | 5,549.14 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 656.45 | 1,094.91 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,402.87** | **40,841.33** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 6,606.15 | 5,476.54 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 336.27 | 1,707.74 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 80.81 | 441.08 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38.25% | 38.16% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.67% | 3.55% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.15% | 75.05% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 47.38% | 44.49% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 93.26% | 91.77% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | -1.11% | -19.93% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | -1.33% | -13.05% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2022 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31 Desemba 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Desemba 2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Desemba 2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,039.64 | 2,434.39 | 8,707.52 | 9,635.81 |
| 2 Gharama za Riba | 722.79 | 805.96 | 3,258.97 | 3,237.67 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,316.85** | **1,628.43** | **5,448.54** | **6,398.15** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 951.18 | - | 951.18 | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 3.12 | (4.82) | 6.27 | 82.90 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **238.90** | **379.58** | **702.49** | **955.34** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 55.30 | 54.75 | 196.93 | 152.73 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 183.60 | 324.83 | 505.56 | 802.60 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **989.92** | **1,025.57** | **3,839.74** | **3,481.01** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 394.37 | 342.02 | 1,633.82 | 1,376.29 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 12.78 | 12.49 | 34.07 | 33.92 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 582.78 | 671.06 | 2,171.85 | 2,070.80 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(388.46)** | **987.26** | **1,353.84** | **3,789.57** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 50.00 | 355.00 | 697.40 | 1,165.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(438.46)** | **632.26** | **656.45** | **2,624.57** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 26 | 25 | 26 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | (13) | 19 | 20 | 80 |
| 13 Mapato kwa Hisa | (13) | 19 | 20 | 80 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.69% | 1.92% | 0.74% | 2.10% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -4.29% | 6.31% | 2.14% | 6.73% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 63.63% | 51.07% | 62.42% | 47.34% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.58% | 5.40% | 6.73% | 5.52% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2022.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2022 | Robo Mwaka iliopita 30 Septemba 2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Desemba 2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Desemba 2021 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (438.46) | 322.26 | 656.45 | 2,624.57 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 97.28 | 97.76 | (21.86) | 402.48 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | (2,420.84) | (282.33) | 1,070.36 | (2,681.41) |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | (708.44) | (15,941.50) | (29,765.88) | 11,776.98 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (152.25) | 229.99 | 888.62 | 753.04 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 403.66 | 2,159.60 | 308.46 | 759.87 |
| Kodi iliyolipwa | (50.00) | (114.06) | (697.40) | (1,165.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(3,269.05)** | **(13,528.27)** | **(27,561.25)** | **12,470.54** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | - | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | 6.27 | (16.18) | 319.16 | (6.03) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 770.64 | 2,651.94 | (6,999.96) | (2,005.73) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **776.91** | **2,635.76** | **(6,680.80)** | **(2,011.76)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | (492.45) | (492.45) | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (72.75) | (70.98) | (280.53) | (254.15) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(72.75)** | **(563.43)** | **(772.98)** | **(254.15)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (2,564.90) | (11,455.94) | (35,015.03) | 10,204.63 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 14,651.03 | 26,106.96 | 47,101.31 | 36,896.83 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **12,086.13** | **14,651.03** | **12,086.28** | **47,101.46** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 31/12/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | - | **6,129.50** | **1,279.37** | - | - | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 656.45 | - | - | - | **656.45** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 971.22 | (971.22) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | - | **7,264.72** | **308.15** | - | - | **40,402.87** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | - | **4,754.21** | **41.35** | - | - | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,613.31 | - | - | - | **2,613.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,238.02) | 1,238.02 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | - | **6,129.50** | **1,279.37** | - | - | **40,238.87** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Desemba 2022**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 23-01-2023 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 23-01-2023 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 23-01-2023 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 23-01-2023 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 23-01-2023 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

# Mwili wa aliyekuwa mfanyakazi wa TBS wazikwa chini ya ulinzi

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA mfanyakazi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Henry Massawe, jana alizikwa chini ya usimamizi wa Jeshi la Polisi Pwani katika eneo alikokuwa akiishi Kiharaka, Kata ya Mapinga mkoani Pwani.

Polisi ililazimika kusimamia mazishi hayo baada ya Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo kuamuru mwili huo kuzikwa katika nyumba yake aliyokuwa akiishi.

Mwili huo umezikwa bila mke wa marehemu, Janeth Ikuyumba, kushiriki na mama mkwe, mtoto wake na msaidizi wa nyumbani wakiwa wamejifungia kwa ndani.

Mfanyakazi huyo wa TBS alifariki Januari 16, mwaka huu, lakini hakuzikwa baada ya kuibuka kwa mgogoro kati ya ndugu zake marehemu na mke wake.

Ndugu walisema kabla ya umauti kumfika, kijana wao alitaka azikwe nyumbani kwake Kiharaka alipokuwa akiishi, lakini mke wake alidai mumewe alitaka azikwe nyumbani kwao alikozaliwa, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Ndugu walipomshinikiza azikwe nyumbani kwake, mke alikimbilia mahakamani kwenda kuweka zuio.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kiharaka, Simoni Kilian, alisema uamuzi wa mahakama wa kuzikwa marehemu huyo ulitolewa jana asubuhi na kuomba ulinzi wa polisi kufanikisha mazishi hayo kwa amani.

"Huyu kijana alikuwa ni mkazi mzuri na mwema kwenye huu mtaa na hata sisi tulishangaa kwa nini hili lilitokea, lakini cha kushukuru limeisha, tumezika kwa amani. Mke wake hakushiriki na hata mama yake mzazi walijifungia ndani na mtoto wa marehemu ambaye mi mdogo kama miaka miwili au mitatu hivi na msichana wa kazi, nafikiri walifanya hivyo kwa hofu."

"Lakini mimi niliwahakikishia kwamba hakuna lolote baya litakalowapata na kuna amani ya kutosha."

Kiliani alisema kabla ya kuingiza mwili ndani walialazimika kuvunja mlango kwa sababu ulikiwa umefungwa kwa ndani na baada ya kumalizia shughuli ya mazishi waliufunga kama walivyoukuta.

Mmoja wa kijana aliyekuwa akifanya kazi na merehemu ambaye hakupenda jina lake litajwe, alisema Henry ameugua kama wiki tatu na mara ya mwisho walikuwa naye jijini Dodoma kwenye mkutano wa kikazi wa Shirika lao katikati ya mwezi Desemba, mwaka jana.

"Tulikuwa tukiwasiliana anasema kwamba anaumwa ndiyo maana haji ofisini kwa siku chache hizo, lakini tukajua sio serious kihivyo."

"Nilichojifunza ni kwamba kuna umuhimu wa kuandika wosia pale tu unapokuwa na familia au kuwa na mali zako. Vijana wengi hatufanyi hivyo tunafikiri ni mpaka uwe mzee ndiyo uandike, hili ni funzo."

Alisema wamebaini Henry na mkewe walikuwa na ugomvi wa muda mrefu.

"Tumekibaini kwamba hawa watu walikuwa na ugomvi wa muda mrefu yeye na mke wake, walifunga ndoa mwaka 2018, lakini inavyosemekena tayari ndoa yao ilikiwa na mgogoro mkubwa," alisema.

"Cha kushangaza Henry hakuwahi kutuambia, yaani ni bora kama angetuambia labda tungejua namna ya kumsaidia. Alikuwa ni mshikaji sana, anacheka sana na watu, mchapakazi."

Mmoja wa majirani, Lucas Mwakapeje, alisema majirani ndio walioshiriki kwa kiwango kikubwa kufanikisha mazishi hayo wakishirikiana na polisi kuvunja mlango wa geti na kuingiza mwili, kuhakikisha umezikwa na kila kitu kimekaa sawa.





**Tangu kampuni ya Barrick** ilipoingia ubia na Serikali ya Tanzania, mwaka 2019, ilijikita katika kufufua na kukuza uzalishaji katika migodi ya North Mara, Bulyanhulu na Buzwagi. Kwa hakika, jitihada hizo zilizaa matunda. Kwani, hadi leo, kampuni ya Barrick iliweza kulipa wanahisa gawio la Dola za kimarekani milioni 311. Aidha, kampuni ya Barrick kwa ujumla imewekeza zaidi ya Dola za kimarekani Bilioni 2.4 katika uchumi wa nchi na kutumia kiasi cha Dola za kimarekani milioni 10.1 katika masuala mbalimbali ya kijamii. Kwa upande wa rasilimali watu, Barrick, imetengeneza ajira mpya 1,842, Hatua hii imefanya asilimia 96 ya wafanyakazi wote migodini kuwa ni Watanzania.

Migodi ya North Mara na Bulyanhulu ipo kwenye njia sahihi kufikia hatua ya daraja la kwanza kweye uzalishaji wa dhahabu *(*Tier 1 Gold Complex)*, ikitokea kwenye udumavu wakati Barrick ikichukua migodi hii na kuelekea kwenye kilele cha sekta hii ya madini.

dPA 6577

BARRICK
Tunajenga Mustakabali
www.barrick.com | NYSE : GOLD · TSX : ABX

** Mgodi wa daraja la juu (Tier One Gold Asset), ni mgodi wenye uwezo wa kuzalisha wakia 500,000 za dhahabu kwa mwaka kwa gharama iliyo chini ya wastani wa gharama za uzalishaji katika sekta ya madini ya dhahabu kwa kipindi cha wa uhai wa mgodi huo ambao ni angalau miaka kumi.*


# Panga la Samia lafyeka wakurugenzi wanne, DC

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune na wakurugenzi watendaji halmashauri nne nchini kuanzia Januari 22, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, walioondolewa kwenye nafasi zao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Msongela Palela.



Mwingine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Linno Mwageni.

Taarifa hiyo ilisema pia Rais ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Ndori.

Aidha, taarifa hiyo haikueleza sababu za kuondolewa kwa viongozi hao, huku ikiwa ni mwendelezo wa kauli ya kiongozi huyo kuwa atafanya mabadiliko ya watendaji wa serikali ambao hawaendani na kasi yake.

MCB BANK BETTER TOGETHER
Mwalimu Commercial Bank Plc

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Dis-2022 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-2022 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 316 | 735 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,056 | 5,033 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 18 | 30 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 41 | 8 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | 1,402 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 5,266 | 9,795 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 64,356 | 57,485 |
| 12. Mali Nyingine | 3,219 | 4,299 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 842 | 893 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **83,114** | **79,680** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | 3,500 | - |
| 18. Amana za Wateja | 60,179 | 60,057 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 951 | 1,606 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 1,265 | 260 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | 92 |
| 27. Dhima Nyingine | 1,406 | 1,702 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **67,301** | **63,717** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,813** | **15,963** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (20,180) | (19,975) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 81 | 26 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,813** | **15,963** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 581 | 581 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (427) | (382) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 19.0% | 20.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.9% | 1.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 100.4% | 95.1% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 76.9% | 71.7% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.8% | 84.4% |
| - Ongezeko la Amana | 6.0% | 8.2% |
| - Ongezeko la Mali | 4.3% | 5.4% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 31-Dis-2022 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Dis-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dis-2022 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dis-2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 2,538 | 1,781 | 8,641 | 5,674 |
| 2. Gharama za Riba | 879 | 576 | 3,192 | 1,783 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,659** | **1,205** | **5,449** | **3,891** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 45 | 71 | 45 | 51 |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 480 | 579 | 1,996 | 1,359 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | - | (1) | 5 | 1 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 367 | 541 | 1,771 | 1,301 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 113 | 39 | 220 | 57 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 2,027 | 1,767 | 7,304 | 6,561 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 755 | 742 | 3,113 | 2,874 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 1,272 | 1,025 | 4,191 | 3,687 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **67** | **(54)** | **96** | **(1,362)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 15 | 23 | 15 | 25 |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **52** | **(77)** | **81** | **(1,387)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | | | | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **52** | **(77)** | **81** | **(1,387)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 58 | 55 | 58 | 55 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 1 | -1 | 2 | -22 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *0.1%* | *-0.1%* | *0.1%* | *-2.4%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *0.3%* | *-0.5%* | *0.5%* | *-8.7%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *94.8%* | *99.0%* | *98.1%* | *127.6%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2.4%* | *2.6%* | *7.8%* | *7.9%* |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mtaji tangulizi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | 16,017 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 81 | - | 81 |
| Mengineyo | - | (285) | - | (285) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,099)** | **5,000** | **15,813** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (18,508) | 5,000 | 17,404 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (1,387) | - | (1,387) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(19,895)** | **5,000** | **16,017** |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Dis-2022 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dis-2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Dis-2021 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | 67 | 26 | 96 | (1,362) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 313 | 313 | 1,244 | 1,329 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,342) | (15,394) | (23,944) | (18,276) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 122 | 14,289 | 21,459 | 19,686 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 4,867 | (1,793) | 3,670 | 357 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 811 | (1,176) | (221) | 156 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | (35) |
| - Mengineyo | (160) | (156) | (300) | (333) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **3,678** | **(3,890)** | **2,004** | **1,522** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | 5 | (15) | (229) | (218) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **5** | **(15)** | **(229)** | **(218)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | 262 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **262** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 3,683 | (3,905) | 1,775 | 1,566 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,134 | 8,039 | 6,051 | 4,485 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 7,817 | 4,134 | 7,826 | 6,051 |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DECEMBA 2022

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ......................... (Imesainiwa) | 24 Januari 2023 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ......................... (Imesainiwa) | 24 Januari 2023 |
| Patrick Mashalla (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ......................... (Imesainiwa) | 24 Januari 2023 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ......................... (Imesainiwa) | 24 Januari 2023 |
| 2/ Enna V. Mwakipesile (Mkurugenzi) | ......................... (Imesainiwa) | 24 Januari 2023 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7,500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1,300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100,000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6,000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40,000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | **Savings Accounts (Disclose for product specific types)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5,000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1,400 |
| | (c) Interim statement | TZS 1,500 |
| | (d) Account closure | TZS 20,000 |
| 3 | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 0.77% p.a |
| | (i) Personal loans | 16% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**

| Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|
| 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.0% | 2.5% |
| 2 - 10Mln | 2.0% | 2.5% | 3.0% |
| 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.0% | 3.5% |
| 50 - 100 Mln | 3.0% | 3.5% | 4.0% |
| 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.0% | 4.5% |
| 300 - 500 Mln | 4.0% | 4.5% | 5.0% |
| 500m - 1Bln | 4.5% | 5.0% | 5.5% |
| Above 1 Bln | Contact Treasury | | |

| Savings Account - TZS | Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly |
|---|---|
| 0- 50k | 0.5% |
| 50k - 1mln | 1.0% |
| 1 - 10mln | 1.5% |
| 10 - 100mln | 2.0% |
| Over 1mln | 2.5% |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 24 Januray 2023 |
| 2 | Leticia Ndongole | Head of Business Development & Marketing | | 24 Januray 2023 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 24 Januray 2023 |

MCB BANK BETTER TOGETHER
Mwalimu Commercial Bank Plc

Ada
Chap Chap

Mkopo wa haraka kwa ajili ya ada ya shule kwa waajiriwa wanaotaka kujiendeleza kielimu au kwa ajili ya kulipa ada za wategemezi wao



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu, kujitoa uhifadhi shoroba ni muhimu kwa maendeleo ya jamii

**SHIRIKA** la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) katika mradi wa Tuhifadhi Maliasili imetenga dola za kimarekani milioni 37.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mapitio ya wanyama (shoroba) ili kuwapo kwa uhifadhi endelevu.

Mradi huo una lengo la kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi shoroba hizo kwa wanyama na wakazi wa maeneo husika ili nao wawe sehemu ya kulinda maeneo hayo ili waweze kuyatumia kwa muda mrefu na kurithisha vizazi vyao.

Kupitia mradi huo taasisi zinazojihusisha na uhifadhi zitapata fedha ya kuendesha miradi kuanzia Dola 200,000 (takribani Sh. bilioni 4.6) kwa mwaka na kama zikifanya vizuri zinaweza kuongezewa mkataba hadi miaka mitatu lengo likiwa ni kuzishirikisha katika uhifadhi huo.

Tunaamini juhudi zinazofanywa kupitia mradi huo, pamoja na juhudi za serikali, jamii na wadau wote wa uhifadhi zitaleta manufaa makubwa kwa serikali, wananchi na wazawa wanaoishi kwenye maeneo yenye shoroba hizo ambazo huchangia kukuza uchumi wao.

Baadhi ya faida wanazopata wakazi wanaoishi maeneo yenye shoroba hizo ni shughuli za utalii kutokana na wanyama wanaopita maeneo hayo, kilimo, pamoja na upatikanaji wa matunda, dawa na maua kutoka kwenye miti iliyoko katika hifadhi hizo.

Ni muhimu pia kuwapo na mipango shirikishi na wazawa katika kutafuta suluhu ya kutunza shoroba hizo ili kuwapo na suluhisho rafiki kwa pande zote mbili na jamii iwe sehemu ya kutunza maliasili hizo kwa kuwa vyanzo vikuu vya kutoweka kwake ni shughuli za kibinadamu na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Shughuli za binadamu kama vile kilimo, ujenzi wa nyumba za makazi katika mapitio hayo zinakuleta usumbufu kwa wanyama hao na kusababisha kuvamia makazi na huku kundi kubwa la binadamu likipata madhara na wanyama kutoweka.


Aidha, uamuzi wa kujikita pia kwenye kuboresha sera na miongozo ya uhifadhi na kutengeneza sera mpya nzuri kwenye maeneo ambayo hayana sera ni wa muhimu kwa sababu utachangia kuwapo na usimamizi mzuri katika maeneo hayo.

Katika ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira mwaka 2022-2032 inaonyesha takribani spishi 2,100 zipo hatarini kupotea ikiwamo mimea 895, wanyama 841 kama hakutokuwa na usimamizi mzuri katika hifadhi zetu na kusababisha baadhi kutoweka ikiwamo shoroba za wanyamapori.

Ripoti hiyo imetaja baaadhi ya shoroba zilizohatarini kuharibiwa na kuwa ni Wami-Mbiki (Hifadhi za Taifa za Saadani, Mikumi na Selous), Kwakuchinja-Mbugwe (Hifadhi ya Taifa ya Tarangire), Mayoka-Magara-Mwada-Vilimavitatu (Hifadhi ya Taifa ya Tarangire), Jangwani (Eneo la Pori la Mto wa Mbu) Kitete- Lositete ya Juu (Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro) na Laja (Hifadhi ya Ngorongoro na Msitu wa Marang).

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa kupitia mradi huo, kama jamii iishio maeneo husika, serikali na wadau wa uhifadhi hawatokuwa na moyo wa kujitoa kusimama katika kuboresha hifadhi hizo itakuwa ni kutwanga maji kwenye kinu kwa kuwa hali ya shoroba itaendelea kuwa mbaya na hatimaye kupotea kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Karibu Lissu leo Mwembe Yanga

**MACHO** na masikio ya wanachama na wapenzi wa CHADEMA wa Dar es Salaam na vitongoji vyake, leo yatakuwa yameelekezwa katika Uwanja wa Mwembe Yanga Temeke, kumsikiliza Tundu Lissu, baada ya kurejea nyumbani.

Katika uwanja huo, kutafanyika mkutano wa hadhara utakaohutubiwa na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Lissu, ambaye anatarajiwa kurejea nchini saa 7:35 mchana wa leo.

Lissu ambaye ni mwanasheria, alipata hifadhi ya kisiasa nchini Ubelgiji baada ya kunusurika kifo tangu mwaka 2017 na sasa anarudi nyumbani kutokana na kile anachoeleza kuwa ni kuwapo kwa mazingira mazuri ya kuendesha siasa.

Mazingira hayo yanatajwa kuwekwa na serikali ya awamu ya sita kwa lengo la kujenga taifa lenye maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na ukuaji wa demokrasia, ambapo katika eneo la maridhiano ya kisiasa, ndipo suala la mikutano ya vyama vya upinzani linapoingia.

Ratiba ya ujio wake inaonyesha kuwa baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere Dar, atakwenda Mwembe Yanga Temeke kuhutubia mkutano huo wa hadhara.

Wakati wanachama na wafuasi wa CHADEMA wakisubiri kwa hamu ujio wa kiongozi wao huyo, si vibaya kukumbushana mambo kadhaa yenye lengo la kusaidia kuendesha siasa zenye manufaa kwa umma.

Kiongozi huyo ni mwanaharakati, lakini ni vyema asije akayumbishwa na wanachama wanaotamani kusikia bazo hufikia 'kuwashambulia' wengine kwa maneno.

Kwa kutumia ushawishi wake wa kisiasa, awasaidie wanachama wenye mihemko ya kisiasa kubadilika ili wajielekeze katika siasa za kistaarabu zinazosaidia kuwaunganisha Watanzania.

Wakati mwingine siasa za aina hiyo hugeuka kuwa za majitaka, hasa kutokana na kuwatukana wanasiasa wengine au kurushia wengine maneno makali, jambo ambalo linaweza kuleta sintofahamu katika siasa za sasa.

Ikumbukwe kuwa marufuku ya mikutano ya hadhara ya kisiasa imeondolewa, na sasa Watanzania wanatamani kusikia hoja zenye majibu ya kutatua changamoto zinazowakabili badala ya kulalamika tu.

Tayari Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe ameshaonyesha njia katika uzinduzi wa mikutano ya hadhara kwa kujikita katika hoja badala ya mashambulizi kwa wengine.

Hivyo, wanasiasa wengine akiwamo Lissu ni vyema wakaiga mfano huo, ili mikutano ya vyama vya siasa iweze kujaa watu wengi wanaosikiliza hoja za viongozi wa vyama hivyo na si kuwakatisha tamaa.

Kwa kuwa Lissu naye anasubiriwa kwa hamu kuhutubia mkutano wa hadhara katika viwanja vya Mwembe Yanga, ni vyema akafuata nyayo za mwenyekiti wake, kwa kujikita zaidi katika hoja za chama hicho.

Mwanasiasa huyo ni miongoni mwa wana CHADEMA wenye uwezo mkubwa wa kujenga hoja, ninaamini kwa njia hiyo ataweza kuteka watu wengi na kuondoa dhana kuwa viongozi wa chama hicho wamezoea kutukana.

Ameitikia wito wa Rais Samia Suluhu Hassan na kuonyesha utayari kurudi nyumbani kuendeleza siasa na pia kushiriki katika mchakato wa katiba mpya, ni muhimu hayo yakafanyika na kuleta matokeo chanya.

Tangu awali wakati anaingia madarakani, Rais ameonyesha utayari wa kukutana na viongozi karibu wote wa vyama vya upinzani na kutoa ruhusa ya mikutano ya hadhara, ilikuwa mojawapo ya mambo aliyoshauriwa kufanya na wadau mbalimbali wa siasa akakubaliana nao.

Kilichobaki sasa ni wanasiasa wenyewe akiwamo Lissu, kutumia nafasi hiyo kunadi sera za chama chake kwa umma wa Watanzania na kufanya maandalizi ya kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Hata Rais anasubiri kuona kile ambacho anatamani kukisikia nacho ni kutamalaki kwa siasa za kistaarabu, huku wanasiasa wakitumia nafasi hiyo kujadili masuala muhimu pasipo kufanya mambo yatakayoharibu amani, utulivu na maadili ya Watanzania.

# Wanafunzi 24,000 Rukwa hawajui KKK

**Na Devota Mwachang'a,** NKASI

ZAIDI ya wanafunzi 24,000 kati ya 300,000 wa darasa la kwanza mpaka la saba wa shule za msingi mkoani Rukwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Ofisa Elimu Mkoa wa Rukwa, Samson Hango, alisema hayo wakati wa kikao kilichoandaliwa na Cambridge Education Tanzania kwa waandishi wa habari, maofisa habari wa halmashauri na viongozi wa radio za kijamii mkoani humo, kilichofanyika Namanyere wilayani Nkasi.

Alisema takwimu hizo zilikusanywa Desemba mwaka jana, kupitia mradi huo ambao ni mpango wa serikali unaofadhiliwa na UK Aid kwenye mikoa tisa Tanzania Bara ili kupunguza idadi ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi bila kumudu KKK.

"Tunaishukuru serikali kwa kuanzisha Mradi wa Shule Bora, natamani sana mradi huu pamoja na kutekeleza afua nyingine, hii ya kuwezesha wanafunzi kumudu KKK tuimalize, tumepewa maagizo na wizara ya TAMISEMI ya kuondoa tatizo hilo, tunapambana kulimaliza ili tuweze pia kupata tuzo za serikali," alisema Hango.

Katibu Tawala mkoa huo, Rashid Mchatta, alisema; "Kimsingi mkoa wetu bado haufanyi vizuri katika elimu kwa ngazi zote kuanzia elimu ya awali, msingi na sekondari, haki hii inachangiwa na mwamko mdogo katika kuunga mkono sekta ya elimu na sababu mbalimbali."

Mchatta alisema juhudi zinahitajika kwa vyombo vya habari vya umma na binafsi kuutangaza mradi ufahamike kwa jamii kwa kuwa umekuwa ni mkombozi mkubwa wa kuimarisha taaluma katika shule za msingi na kuinua elimu.

Mratibu wa Mradi kutoka Cambridge Education Tanzania, John Shindika, alisema wataalamu wa mradi huo na serikali walishirikiana, kupitia na kubaini afua 10 ambazo zilikubaliwa kutekelezwa kwa pamoja.

"Mradi umeiwezesha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuratibu mafunzo endelevu kazini kwa walimu yanayozingatia mwongozo wa mpango endelevu wa walimu kazini - MEWAKA, ambayo yatafanyika kwa awamu tatu katika Halmashauri za Nkasi na Sumbawanga Manispaa," alisema.

Shindika alifafanua mafunzo yatahusisha maofisa elimu kata 47, walimu wakuu 169, walimu wa taaluma 169, walimu mahiri waelimishaji rika 338 na maofisa udhibiti ubora wa shule (2), maofisa taaluma msingi (2) na katibu tume ya utumishi wa walimu (2).

Mradi huo unatekelezwa kwa miaka sita kuanzia Aprili 2021 hadi 2027 katika mikoa ya Tanga, Pwani, Mara, Simiyu, Singida, Dodoma Kigoma, Rukwa na Katavi kwa ushauri wa Kitaalum kutoka Cambridge Education ikishirikiana na Action for Disability and Development (ADD) International, International Rescue Committee na Plan International.

# Katekista kortini tuhuma kubaka mwanafunzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KATEKISTA wa Kanisa Katoliki, Parokia ya Mlangali wilayani Ludewa, Simon Njavike (43), amepandishwa kizimbani katika mahakama ya wilaya hiyo kwa kosa la kumbaka mwanafunzi wa kidato cha tatu (17).

Akisomewa shtaka hilo na Mwendesha Mashtaka, Angelo Marco, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya Ludewa, Isaac Ayengo, imedaiwa mshtakiwa huyo ni mwalimu wa watoto wa kipaimara na binti huyo ni mmoja wa wanafunzi wake aliyekuwa akifanya vizuri katika mafunzo hayo. Imedaiwa Katekista huyo alimpa Sh. 10,000 kama zawadi ya kufanya vizuri kwenye mafunzo hayo.

Mahakama hiyo ilielezwa kuwa baada ya siku kadhaa mshtakiwa huyo alianza kumtaka kimapenzi, lakini binti huyo alikataa, ndipo akaanza kudai kurudishiwa Sh. 10,000 aliyokuwa amempa, lakini binti alishindwa kuirudisha kwa kuwa hakuwa nayo.

Alidai kuwa baada ya siku kadhaa mshtakiwa huyo alimwita binti nyuma ya kanisa ambako kuna kichaka majira ya mchana na binti alipofika alimkamata kwa nguvu kutimiza lengo lake hilo na kutokomea kusiko julikana.

Polisi ilimtia mbaroni baada siku kadhaa za kutoroka. Mshtakiwa huyo amekana shtaka hilo na kesi hiyo imahirishwa hadi Februari 9, mwaka huu, itakapotajwa tena.




Meneja wa Benki ya Biashara Tanzania tawi la Mbagala, Edward Mwoleka (wa tatu kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa mifuko 150 ya simenti kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kilamba, Leah Masaba, iliyotolewa na benki hiyo, mkoani Dar es Salaam hivi karibuni. Kutoka (kulia) ni Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano TCB, Gloria Mutta, Diwani wa Kata ya Charambe, Twahil Shaban na Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Betha Minga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawili mbaroni tuhuma kuvua samaki kwa baruti kilo 980

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji jijini Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa wawili wanaodaiwa kukutwa na samaki kilo 980 wanaosadikika kuvuliwa kwa baruti. Kamanda wa kikosi hicho, Moshi Sokoro, alisema jana kuwa samaki hao wamekamatwa wakiwa kwenye boti ya uvuvi yenye namba za usajili Z 103585 MV Maedra.

Alisema wamekamatwa Januari 12, maeneo ya Soko la Samaki Feri baada ya operesheni kufanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Kamanda Sokoro aliwashukuru wananchi wanaochukia uhalifu na kuwaomba waendelee kutoa taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema Jeshi la Polisi litachukua hatua kwa yeyote atakayehusika na uvuvi haramu pamoja na makosa mengine ya jinai.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED






Baadhi ya watoto wenye mahitaji maalum wanaotunzwa na Baba Oreste Foundation, wakipata chakula cha mchana wakati Kampuni ya Dough Works Limited, ilipofungua rasmi mgahawa wa KFC & Pizza Hut, eneo la Mbezi Beach kwa Zena, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 86.2/- kuboresha mapitio wanyamapori

**Na Jenifer Gilla**

ZAIDI ya Dola za Marekani milioni 37.5 sawa na (Sh. bil 86.25) zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mapitio ya wanyama (shoroba), pamoja na kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari kwa ajili ya kuwa na uhifadhi endelevu kwa manufaa ya binadamu na wanyamapori.

Hayo yameelezwa hivi karibuni wilayani Bagamoyo mkoani Pwani na Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) katika mradi wa Tuhifadhi Maliasili, John Noronha, wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari za mazingira yaliyotolewa na Chama cha Waandishi wa Mazingira (JET) kupitia mradi huo.

Akiutambulisha mradi huo John alisema ni wa miaka mitano unaofadhiliwa na mradi wa USAID Tuhifadhi Mazingira, ukilenga uhifadhi wanyamapori ambapo mwaka huu umejikita kuangalia changamoto zilizoko katika shoroba hizo kuzitatua kwa ajili ya uhifadhi endelevu wa maliasili hususani wanyama pori.

Aidha, alisema katika fedha hizo Dola milioni saba (Sh. bil 16.1), zitatumika kutoa fedha za kutekeleza miradi ya uhifadhi wanyamapori, taasisi itakayoshinda zabuni itapewa kuanzia Dola 200,000i (Sh.bil 4.6) kwa mwaka na akifanya vizuri anaweza kuongezewa mkataba wa miaka mitatu.

"Ulianza Julai, 2021 na mpaka sasa upo katika mwaka wa pili, na una malengo makuu matatu ikiwamo kujengea uwezo wadau, taasisi za kiserikali, binafsi na vyuo kwa kuwapa elimu fedha na vitendea kazi kama kompyuta ili kutekeleza miradi ihusuyo uhifadhi," alisema.

Alisema lengo la pili ni kuzihusisha taasisi binafsi zinazohusika katika uhifadhi wa wanyamapori zikiwano kampuni za utalii ili wawe sehemu ya utunzaji wa hifadhi kwa kuwa zimekuwa zikiachwa nyuma.

Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi wa mradi huo, Dk. Elikana Kalumanga, alisema elimu ya uhifadhi wanyamapori inawafikia makundi yote muhimu na wameungana na JET kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari.

"Kwenye haya maeneo yote tumejitahidi sana kushirikisha wadau wengi ikiwamo JET, ili kuwapa waandishi habari mafunzo kwa sababu kuna baadhi ya maeneo hatuna utaalamu nayo kwa hiyo tutaajiri kampuni za kutusaidia kutoa mafunzo," alisema.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema kupitia mradi huo waandishi wa habari watafundishwa mada mbalimbali zihusuzo uhifadhi wa mapitio ya wanyama na kuandika habari za kuelimisha jamii umuhimu wa kuhifadhi shoroba.

"Baada ya mafunzo haya, waandishi watatembelea shoroba saba ikiwamo Kwakuchinja inayounganisha Tarangire na Manyara, Amani -Niru, iliyopo Muheza, Nyerere -Selou na Odungwa, Ruaha-Rungwa-Inyonga na Ruaha-Rungwa-Katavi," alibainisha John.

# Adaiwa kujinyonga kisa msongo wa mawazo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, Juma Mohamedi (52), amedaiwa kujinyonga kwa kamba kutokana na msongo wa mawazo baada ya kifo cha dada yake.

Taarifa zinadai Mohamed alichukua uamuzi huo baada ya kifo cha dada yake, Nuru Ahmadi (60), aliyeugua kwa muda mfupi.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Namayuni wilayani Kilwa, Ally Mtumbuka, alisema Mohamedi alifika kijijini hapo Januari 16, mwaka huu baada ya kupata maelezo ya kifo cha dada yake na kupelekwa makaburini kuona kaburi.

Alisema baada ya kuona kaburi, alimwombea dua dada yake huku akiwa analia.

"Wakati anaomba dua alikuwa akitokwa na machozi na baadaye alisema ameondokewa na mshauri na mtegemezi wake mkubwa aliyekuwa akisaidiana naye katika majukumu mbalimbali ya kimaisha," alisema Mtumbuka.

Kadhalika, alisema kutokana na hali hiyo siku zote alizokuwapo kijijini hapo, alikuwa kwenye msongo wa mawazo.

Alisema Januari 18 aliaga wenzake kuwa anakwenda kulala nyumbani kwa mjomba wake.

"Baada ya kupiga simu kwa mjomba wake kuulizia kama Juma amefika, majibu yalikuwa bado hawajamwona," alisema Mtumbuka.

Alisema ndugu na majirani walianza kumtafuta na saa 7:00 usiku walimkuta akining'inia juu ya dari la banda la nyumba kubwa la marehemu dada yake, akiwa amejinyonga kwa kamba.

Mtumbuka alisema, walitoa taarifa Polisi na Mganga wa zahanati ya kijiji, Dk. Ernest Sanka, ambaye aliufanyia uchunguzi mwili na kutoa ruhusa ya ndugu na jamaa kuzika.

Dk. Sanka alisema kifo chake kilichangiwa na msongo wa mawazo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Pili Mande, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na wanaendelea na upelelezi.

# Aliyepata ajali awaomba Watanzania kumsaidia mtaji

**Na Romana Mallya**

NI mtihani baada ya kijana Ramadhan Misego (41) mwenyeji wa Kibungo, Kungwe mkoani Morogoro (pichani), aliyekuwa mfanyabiashara wa soko la Buguruni, ndoto yake kuzima ghafla baada ya ajali iliyomsababishia majeraha makubwa kichwani.

Kijana huyo aliyefika jana ofisi za Nipashe, Mikocheni mkoani Dar es Salaam, amewaomba wasamaria kumchangia Sh. 300,000 za mtaji wa kuuza nguo za wanawake aina ya vijora.

Alisema alipata ajali eneo la Buguruni miaka mitatu iliyopita wakati akivuka barabara.

Ajali hiyo ilisababisha afanyiwe operesheni ya kufumuliwa kichwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kwa sasa anakwenda kliniki kuchukua dawa za mwezi au miezi miwili.

Alisema baada ya matibabu hayo amekuwa akiishi katika mazingira magumu kutokana na kutegemewa na mke na watoto wake wawili ambao kwa sasa wapo kijijini mkoani Morogoro.

"Ajali ilitokea mwezi Machi mwaka 2021 eneo la Buguruni Sokoni, gari iliyonigonga eneo la tukio baada ya watu kupiga kelele kuwa, 'umeua' dereva wakati akikimbia alinigonga tena mguu wa kushoto na kuondoka.

"Hivyo, nilipata mama mmoja msamaria ambaye ndiye aliyenisaidia gharama za matibabu yangu hospitali ya Muhimbili. Baada ya maisha kunipiga mwaka jana mwezi Mei niliamua kuuza simu yangu kwa gharama ya Sh. 40,000 nikapata mtaji wa biashara ya vijora."

Alisema ilipofika mwezi Septemba akiwa ameongeza mtaji wake na kufikia Sh. 95,000, kwa bahati mbaya alipoteza fedha hizo alizokuwa ameweka kwenye mfuko wa suruali wakati akitoa simu mfukoni.

"Nimekuja hapa kuwaomba Watanzania wenzangu wanisaidie Sh. 300,000 kwa ajili ya kuendelea na biashara yangu ya vijora au kwa wanaoweza kunipatia vijora kama mtaji, nitashukuru sana," alisema.

Kijana huyo alisema amekuwa akija Dar es Salaam kila baada ya mwezi au miezi miwili kwa ajili ya kliniki yake.

"Dar es Salaam huwa ninafikia kwenye baa ya mama mmoja anayeishi maeneo ya Tandale, kutokana na ugumu wa maisha mama huyu amekuwa akinilipisha Sh. 2,000 kwa ajili ya malazi, huwa ninalala ndani ya baa yake," alisema.

Kwa yeyote aliyeguswa na kijana huyo anaweza kumsaidia kwa namba yake ya simu 0622 052282 au 0694694479 jina ni Ramadhan Juma Misego.







## Madiwani wapitisha rasimu mpango wa bajeti bil. 30/-

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

BARAZA la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, limepitisha rasimu ya mpango wa bajeti ya Sh. bilioni 30 kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Rasimu ya bajeti Sh. bilioni 30 imeongezeka kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.159 sawa na asilimia 4.1 ya bajeti ya mwaka 2022/2023 iliyokuwa Sh. bilioni 28.8.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Simanjiro, Happiness Masatu, aliwasilisha jana rasimu ya bajeti hiyo mbele ya Baraza la Madiwani jana kwenye makao makuu ya wilaya hiyo, Mamlaka ya Mji mdogo wa Orkesumet.

Alitaja baadhi ya miradi ya wananchi itakayonufaika na bajeti hiyo ni kuwezesha Sh.milioni 99 kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Alitaja miradi mingine ni kujenga bweni katika Shule ya Msingi Saniniu Laizer kwa Sh. milioni 60, zahanati ya Olchoronyori, Sh. milioni 10 na Shilingi milioni sita kwa shule shikizi ya Songoyo Loiborsoit.

Alisema Shilingi milioni nne zitatumika kukamilisha vyoo Shule ya Sekondari Tanzanite, Sh. milioni 10 kukamilisha ujenzi wa nyumba Shule ya Msingi Naisinyai na Sh. milioni 10 kukarabati vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Songambele.

"Pia Sh. milioni 40 zitakuwa za vitambaa vya mifugo kuzuia mbung'o, Sh. milioni 10 kwenye ujenzi wa choo Sekondari ya Loiborsiret na ukamilikaji wa maabara ya Shule ya Sekondari Mirerani B.W. Mkapa kwa Sh.milioni 8.5 milioni," alisema.

Hata hivyo, alisema Sh. milioni 10 zimetengwa kwa ajili ya Shule ya Sekondari Eng'eno, Sh. milioni 10 ukamilikaji wa nyumba ya walimu shule shikizi ya Irkinen Gunge na Sh. milioni 10 sekondari Langai.

Sh. milioni 10 zimetengwa kwa ajili ya ukamilikaji wa nyumba ya walimu wa Shule ya Msingi Ormot, Kijiji cha Namalulu na Sh. milioni 10 ukamilikaji wa madarasa Shule ya Msingi Losinyai.

"Kadhalika Shilingi milioni tano zimetengwa kwa ajili ya ukamilikaji wa madarasa shule ya msingi Ngii iliyoko Kata ya Kilombero na Sh.milioni 10 zitakuwa za ujenzi wa jiko Shule ya Sekondari Nyumba ya Mungu," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, aliwasisitiza madiwani kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza tija kwenye miradi ya maendeleo.

Naye Diwani wa Kata ya Orkesumet, Sendeu Laizer, aliomba baraza hilo kubadili matumizi ya Sh. milioni 15 za ujenzi wa vyoo Shule ya Sekondari Simanjiro ili kujengea uzio wa shule hiyo.

# Bima ya Afya kwa Wote kudhibiti wizi, udanganyifu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imesema kuwa Bima ya Afya kwa Wote itadhibiti wizi na udanganyifu kwa kuwa kutafungwa mifumo ya kisasa ili kubaini zahanati, vituo vya afya na hospitali zitakazofanya hujuma.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, wadau wa afya na viongozi wa dini.

Dk. Magali alisema, Wizara ya Afya imejipanga kuongeza vifaa tiba ili kuboresha huduma kwa wagonjwa.

Kitakachofanyika mtu akichangia kwa siku hiyo, aanze kupata huduma pamoja na wategemezi wake.

Alisema wananchi wasiokuwa na uwezo watawezeshwa kupata huduma kupitia Mfumo wa Bima ya Afya au kwa utaratibu wa msamaha baada ya kutambuliwa.

"Kwa kuanza asilimia 30 watasajiliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa kugharamiwa na serikali na asilimia 70 watapatiwa vitambulisho vitakavyowawezesha kupata huduma zitakazofungamanishwa," alisema Dk. Magali.

Aliyataja mambo muhimu yatakayozingatiwa kwenye muswada huo, kuwa ni kitita cha mafao ya huduma muhimu ambacho kila skimu ya bima ya afya italazimika kukitoa na kitakuwa haki ya kila mwanachama.

Alisema kitita hicho kitakuwa na ada ya uandikishaji, kumwona daktari, gharama za vipimo, dawa za aina zote muhimu, upasuaji mdogo na mkubwa, kulazwa, huduma ya afya ya kinywa na meno, matibabu ya macho, vifaa saidizi na huduma za mazoezi ya viungo.

Alitaja mambo mengine ni mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa kuwa itaimarishwa na kuwezesha usimamizi, serikali kutenga fedha na kuziweka kwenye akaunti maalumu kwa ajili ya kugharamia wananchi wasiokuwa na uwezo na makundi maalumu. "Kaya za watu sita zitaundwa na mwanachama na mchangiaji, mwenza na wategemezi wanne," alisema.

Vile vile, alisema bima hiyo, itampa Mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya kuboresha mifuko ya Bima ya Afya ya umma.

Mifuko hiyo itampa mamlaka Waziri wa Afya kutoa kwa kampuni binafsi za bima kufanya tathmini ya uhai na uendelevu kila baada ya miaka mitatu na kufuatwa kwa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na Mfuko wa Bima ya Afya iliyoboreshwa (iCHF) kwa kuanzisha kitita cha mafao ya huduma za msingi za jamii.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Caroline Mthapula, alisema ni wajibu kwa viongozi kutoa elimu kwa umma juu ya muswada wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema watakuwa mstari wa mbele kuhamasisha bima ya afya kwa wote.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kushoto), akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, baada ya kupitisha rasimu ya mpango wa bajeti ya Sh. bilioni 30 kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## H'mashauri yavifutia usajili vituo 19 vya kulea watoto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, imesema imevifutia usajili vituo 19 vya kulea watoto kati ya 22 vilivyoko wilayani humo.

Kufutwa kwa vituo hivyo kumetokana na utafiti uliofanywa na kubaini kuwa vilianzishwa bila kufuata sheria, kanuni na utaratibu na vingine kuanzishwa kwa maslahi binafsi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Hai, Helga Simon, alitangaza hatua hiyo jana wakati wa uzinduzi wa kituo cha watoto yatima cha Kao la Amani kilichojumuisha watoto 32.

Alisema kufungwa kwa vituo hivyo ni kufuatia operesheni maalumu iliyofanywa kwa lengo la kukagua na ilibainika kuwapo kwa vituo ambavyo havikufuata sheria utaratibu na kanuni za nchi wakati wa uanzishwaji.

"Vituo vilivyofutiwa usajili havikuwa na sifa ya uendeshaji, vingine vilikuwa vinaendeshwa kwa maslahi binafsi na wengine kuchukua watoto wa ndugu jamaa na marafiki na kuwahifadhi kwenye nyumba hizo, huku wengine wakiwa na nyumba nyingi ambazo walishindwa kuzisajili kama vituo vya kulea watoto."

Alisema serikali inaamini vituo vya watoto ni sehemu ya mwisho ya kuwalea ikiwa watakosa eneo jingine la kuishi japokuwa wamekuwa wakisisitiza watoto kulelewa nyumbani ili kupata furaha na amani.

Askofu wa Kanisa la EAGT Kanda ya Kaskazini, Barnabas Rashid, akihubiri katika ibada, amewataka watu wenye uwezo, kujitokeza kuwasaidia wahitaji wakiwamo yatima ili kuhakikisha wanapata elimu bora na kuondokana na utegemezi.

Akisoma risala ya kituo hicho, Esther Tukai, alisema kwa sasa kituo hicho kina watoto 32 ambao wamepokewa kutoka maeneo mbalimbali na hupatiwa huduma mbalimbali ikiwamo haki ya msingi ya kupata elimu bora na malazi.

Alisema kituo mpaka sasa kimeshawahudumia watoto 150 na kina maeneo makuu mawili ya kuhudumia wasiojua ndugu zao.

Mkurugenzi wa Kituo hicho, Cletus Tukai, alisema lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuisaidia jamii ya watoto wanaokabiliwa na matatizo mbalimbali katika familia zao na wasiofahamu ndugu zao.

"Utafiti unaonyesha kwenye jamii kuna watoto wengi wenye ndoto za kufika mbali, lakini inashindikana kutokana na kukosa malezi bora ya wazazi au matatizo ya kifamilia na tunakabiliana na matukio ya ukatili kwa kuwaelimisha watoto na walezi wao, tunafanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuwaombea ili kusanyiko lao liwe kwa ajili ya faida na kufikia malengo," alisema Tukai.

Akizindua Kituo cha Kao la Amani, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando, alisema sasa kumekuwa na ongezeko la matukio ya ubakaji na ulawiti katika jamii na ili kumaliza tatizo hilo, wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto maadili mema na kuwajengea hofu ya Mungu.



# Mbowe atambulisha makomandoo wake

**Na Richard Makore,** MWANZA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewatambulisha hadharani makomandoo wake wanaomlinda ambao walikuwa wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), katika mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika juzi jioni mjini Tarime mkoani Mara.

Mbowe alisema makomando hao waliaminiwa JWTZ, lakini alipowachukua na kuwa walinzi wake walipewa kesi ya ugaidi.

"Njooni hapa wawaone, hawa ni makomandoo wa jeshi, ambao tulipewa nao kesi ya ugaidi na kulazimika kukaa wote gerezani," alisema Mbowe.

Alitoa utambulisho huo juzi jioni katika mkutano wa hadhara wilayani Tarime, mkoani Mara alipohutubia wananchi huku akibainisha kazi ya kujenga demokrasia haijawahi kuwa rahisi.

Alisema katika safari yake ya kujenga demokrasia pamoja na siasa amepitia milima na mabonde mpaka kufikia sasa.

"Nataka niwatambulishe kwenu makomandoo wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambao walisingiziwa kesi ya ugaidi na wakakaa gerezani bila hatia," alisema. Baada ya utambulisho huo, wananchi walilipuka kwa shangwe katika mkutano uliofanyika juzi mjini Tarime.

Alisema kazi ya kujenga demokrasia imepitia safari ndefu na ameendelea kupitia milima na mabonde tangu alipoianza.

"Ni safari ya milima na mabonde katika kujenga demokrasia hapa nchini, kwa miaka saba tulikuwa gizani, hatukuweza kukutana kama hivi, bali labda kukutana misikitini, kwenye makongamano ya dini, lakini sasa tunakutana kama hivi," alisema.

Alisema Watanzania wanahitaji Katiba ambayo itamdhibiti Rais kwa kuwa na yeye ni binadamu ili akikosea aambiwe amekosea.

Aliwataka wananchi kuendelea kujenga umoja na mshikamano bila kulipiza kisasi kwa wenzao wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kuhusu viongozi mbalimbali wastaafu, alisema Katiba inazuia kushtakiwa huku akisema jambo hilo halikubaliki na kwa kuwa kiongozi aliyefanya makosa lazima ashtakiwe.

Alitaka Katiba mpya ambayo itawathibiti viongozi hao, kulingana na makosa watakayokuwa wamefanya wakiwa madarakani.

Mbowe alisisitiza CHADEMA sio chama cha visasi na kutaka wanachama wao waendelee kuheshimu askari wa Jeshi la Polisi.

Kuhusu mapokezi ya Makamu wa Mwenyekiti wa CHADEMA, Tindu Lissu, Mbowe alisema atapokewa jijini Dar es Salaam leo.

Wakati huo huo, Mbowe aliwaomba radhi wanawake kwa kuwaita mademu katika mikutano yake na kwamba haoni aibu kuomba msamaha.

"Naombeni mama zangu mnisamehe kama niliwakwaza katika kauli yangu niliyotumia kwa kuwa chama hiki hakioni aibu kuomba radhi," alisema.

Mbowe aliongoza mikutano katika aeneo mbalimbali Kanda ya Ziwa, ikiwamo Mwanza, Lamadi, Bunda, Kiabakari, Musoma mjini na Tarime mjini.



Waumini wa Kanisa la Waadventista Wasabato Shinyanga Mjini, wakiwa kwenye kuhitimisha siku 10 za maombi ya kurejea madhabahuni pamoja na kuliombea Taifa amani na Watanzania kumrudia mwenyezi Mungu na kuacha kutenda maovu ikiwamo kuuana kikatili, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mtumishi chuo cha serikali jela kwa wizi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

ALIYEKUWA mtumishi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii wilayani Kaliua mkoani Tabora, Mdaki Adam, amehukumiwa kwenda jela miaka minne baada ya kutiwa hatiani kwa wizi wa zaidi ya Sh. milioni 19.

Adhabu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Tabora, Jovitty Katto, baada ya kuridhika na ushahidi wa mashahidi wanane wa Jamhuri pamoja na kamera za CCTV za benki ya NMB.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Katto alisema, mahakama imemuona mshtakiwa ana hatia kutokana na ushahidi mbalimbali uliotolewa dhidi yake.

"Ulitumia uaminifu wako vibaya kwa kuendelea kutumia fedha za chuo baada ya mtu aliyekuwa amekabidhiwa kumiliki kadi ya akaunti ya benki ya chuo kufariki," alisema Hakimu Katto.

Alisema vitendo vya uhalifu wa aina hiyo vinatia uchungu kwa mtu aliyekuamini na unapomdhihaki ili aonekane ni mbaya katika jamii baada ya kupata umauti.

Alibainisha kuwa kitendo kilichofanywa na mshtakiwa ni kibaya kwa kuwa kilisababisha chuo kupata mwanguko wa kiuchumi hadi kushindwa kulipa mishahara ya watumishi na chakula cha wanafunzi.

Awali, Wakili wa Serikali, Joseph Mwambwalulu, aliiambia mahakama hiyo kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa nyakati tofauti kati ya Machi 28, mwaka 2021 hadi Mei 26, mwaka 2021.

Mwambwalulu alidai kuwa kwa nia ovu mshtakiwa aliiba Sh. milioni 19 kwa kutumia kadi ya benki kutoka kwenye akaunti namba 90110000683 ya chuo hicho kilichoko wilayani Kaliua mkoani Tabora.

Alidai mshtakiwa kutenda kosa hilo kutoka matawi mbalimbali ya benki ya NMB katika maeneo tofauti ya Mwanza, Tabora, Geita, Rorya mkoani Mara na Manyoni mkoani Singida.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alipewa kadi ya benki na namba ya siri ili awe anamsaidia kutoa fedha mkurugenzi wa chuo ambaye kwa sasa ni marehemu walipokuwa safarini kwa ajili ya matibabu.

Katika utetezi wake ili apunguziwe adhabu, mshtakiwa aliomba aonewe huruma ikiwa ni pamoja na kumpa kifungo cha nje ili aweze kuihudumia familia yake yenye watu zaidi ya wanane wanaomtegemea.

## Wanafunzi watoa kilio taulo za kujistiri

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wanafunzi wa kike mkoani hapa wameomba serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwapatia taulo za kike katika kipindi cha wiki moja ya hedhi ili kuwasaidia kuendelea na masomo yao kutokana na baadhi yao kukatisha masomo kutokana na tatizo hilo.

Wakieleza tatizo hilo la upatikanaji wa taulo hizo juzi, baadhi ya wanafunzi wilayani Kwimba, mkoani Mwanza, walisema kutokana na ukosefu wa fedha kwa familia za wanafunzi hao wanashindwa kuendelea na masomo katika kipindi wanachokuwa kwenye hedhi.

"Taulo zilizoko shuleni ni chache kulinganisha na idadi ya wanafunzi wenye uhitaji wa taulo hizo hali inayosababisha kukosa masomo katika kipindi hiki muda mwingine lazima uende kwa mwalimu mlezi ili upatiwe taulo hizo kila siku," alisema Saraphina Elias mwanafunzi wa kidato cha nne

Shamimu Salumoni, mwanafunzi wa kidato cha tatu alisema kwa wanafunzi wenye uhitaji wanatakiwa kupatiwa taulo zao kulingana na muda wa hedhi ambao mara nyingi unakuwa siku saba.

Zakiah Shakiru, alisema wanafunzi hao wakiwa katika kipindi cha hedhi hukosa raha wakati wa masomo hali inayosababisha kushindwa kuendelea na masomo mpaka muda wa siku saba kama hawana taulo za kike.

Awali, akisoma mpango wa kuwasitiri wanafunzi kwa taulo za kike, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza, Happiness Msange, alisema wametenga Shilingi milioni nane kwa mwaka kwa ajili ya taulo hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alizitaka halmashauri kutenga kiasi cha Sh. milioni 30 hadi Sh. milioni 50 kwa ajili ya kutoa kununulia taulo hizo na kuzigawa katika shule mbalimbali.



Ukurasa 12

## Ujio mikutano ya vyama, UVCCM tutafanya haya



Ukurasa 13

Dimwa awapa raha wana CCM, ahadi ya 90% ushindi 2025



Ukurasa 14

## Putin amebakia kuwatumbua makamanda, vita ikimwelemea


# siasa

JUMATANO JANUARI 25, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


SAMIA KUONGOZA AFRIKA DAVOS

# Ni ishara kukubalika kitaifa, kimataifa, maridhiano, usawa kijinsia vyampaisha

**Na Nimi Mweta**

BILA shaka wachambuzi wa masuala ya uongozi na siasa za kiuchumi barani Afrika na kwingineko, wanakubali kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, amestahili kuongoza ujumbe wa pamoja wa Afrika wa kongamano la jukwaa la biashara na uchumi duniani (WEF) la kila mwaka, huko Davos Uswisi.

Kongamano limefanyika wiki iliyopita ambako awali ilitazamiwa ujumbe huo wa pamoja ungeongozwa na Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini akisaidiwa na Rais Samia.

Hata hivyo, migogoro nchini Afrika Kusini ilimkwamisha Ramaphosa kusafiri, akabaki nyumbani kushughulikia tatizo la umeme, badala ya kuwaachia wasaidizi wake, kama Waswahili wasemavyo anayevaa kiatu anajua kinabana wapi, hivyo ilikuwa vyema kubaki nyumbani.

Kadhalika, amekuwa na wakati mgumu kuhusiana na upotevu wa mamilioni ya dola shambani mwake siku za nyuma na kura ya kutokuwa na imani naye kutokana na kanuni za nidhamu za chama tawala cha ANC ilimhusu.

Kuwapo kwa utulivu katika siasa nchini na kuanza kutekelezwa kwa mpango wa maridhiano unaofungua mlango wa mikutano ya vyama vya upinzani iliyozuiliwa kwa miaka saba kumpa Rais nafasi zaidi anga za kimataifa.

Aidha, ikiwa ni nyongeza muhimu ya sera za uwazi, kuondoa vizuizi vya biashara Jumuiya ya Afrika Mashariki na kukubali Soko Huria la Afrika, ni vielelezo kadhaa vya sifa za Rais Samia kuongoza ujumbe wa AU.

Tangu alipoingia madarakani ametembelea zaidi Afrika akifika Uganda, Kenya, Rwanda, Malawi, Msumbiji, Misri, Ghana. Amezuru Marekani, Qatar na Uingereza, China na Oman.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza katika mkutano wa masuala ya nishati, Davos, nchini Uswizi. **PICHA: IKULU**

Yako maeneo mawili ambako uamuzi wa kumwomba Rais awe kiongozi mwenza wa ujumbe wa pamoja wa Afrika inawezekana yalifanyika, mosi ni mkutano wa wakuu wa nchi wanaokutana Addis Ababa makao makuu ya UA au katika mikutano ya mara kwa mara ya mabalozi wa Afrika katika Umoja wa Mataifa.

Huenda, wanakuwa na vikao vya kujiweka au kuwekana sawa kwa mazungumzo katika kamati za idara na mashirika tofauti ya UN iwe ni kupata mwakilishi kwa mfano kubadilisha walioko Baraza la Usalama na mengine ambako wawakilishi wa kanda hubalishana mawazo.

Hapo pia wangeweza kufikia uamuzi kuhusu mkutano wa Davos endapo suala hilo lingeangaliwa kama la Umoja wa Mataifa, tofauti na AU yenyewe.

Hata suala la kuwa na kiongozi wa pamoja au washirika wawili kuwa viongozi wa pamoja katika mkutano huo kwa upande mwingine halikuwa suala la kiutaratibu tu ila pia la kisiasa.

Ingebidi apatikane kiongozi au viongozi wa kuwakilisha msimamo ambao wajumbe wa Afrika katika taasisi tofauti za kibiashara na uchumi za UN wasingekuwa na tofauti na misimamo ambayo wangechukua.

Ni suala moja kuona umuhimu wa uwakilishi au uwepo wa ujumbe wa pamoja na ni jambo jingine kukubaliana hoja hiyo, kwani inabidi kwanza apatikane kiongozi ambaye wengine hawamtilii shaka, anayekubalika na mwenye vigezo stahiki, ashirikiane na mwingine.

Sura tofauti za Afrika ziwe zimewakilishwa, kwa mfano katika kujadili uwekezaji, tabia nchi, usawa wa jinsia au demokrasia huko Davos, Rais Ramphosa alipewa kijiti kwani nchi yake ni kubwa kiuchumi na kidemokrasia ila yako maeneo wakaona ni Rais Samia atayasimamia vyema. Ni usawa wa kijinsia, moyo wa maridhiano, haki na uhimilivu wa kisiasa.

Inatosha kusema kuwa yapo maeneo ambayo kama si yeye, Afrika haitaonekana katika uhalisia wake na hapa kuna masuala ya uwezo wa wanawake kuongoza, ikiwa inafahamika kuwa ni nadra kwa Afrika na hata kwingineko ila baadhi ya mataifa Ulaya Kaskazini na Australia au ukanda wa Pacific, kuwa na kiongozi mkuu mwanamama.

Hilo lilimpa nafasi Rais Samia ila si haba kuwa anafahamu masuala ya taasisi za fedha za kimataifa na amefanya kazi nazo kwa miaka kadhaa, halafu ana historia ya utetezi wa haki za binadamu hasa akiwa kijana.

INAENDELEA UK. 12

# Ujio mikutano ya vyama

## • UVCCM yatangaza kufanya makubwa kuibua ilani upya, si kujibu mawe ya wapinzani

Na Victoria Mwanziva

DEMOKRASIA kwa tafsiri inayoeleweka na wengi ni mchakato ambao hutoa mwangaza na mwongozo wa namna ya uendeshaji wa mambo katika nchi kuendana na matakwa ya wananchi kisiasa, kiuchumi, kijamii lakini kwa kufuata mila na desturi za nchi na yote hayo yanahusisha ushirikishwaji wa wananchi.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameonyesha nia na dhamira yake ya kuihuisha demokrasia ya Tanzania katika njia ya maridhiano, hivyo sisi vijana wa CCM inatupasa kuunga mkono juhudi hizi kwa ukamilifu kwa kueleza mambo makubwa yanayofanywa na awamu ya sita kupitia Ilani ya Uchaguzi.

Nichukue fursa hii kuwapongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwahudumia Watanzania na Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2020-2025.

Lakini pia kipekee ni wapongeze Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM, Mohamed Kawaida na Makamu Rehema Omari pamoja na Katibu Mkuu Kenani Kihongosi kwa namna wanavyochapa kazi.

Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ipo katika hatua mbalimbali za kutanua wigo wa ushirikishwaji wananchi kwa kuzingatia mazingira ya taifa letu, huku tukiongozwa na moyo wa maridhiano yaliyoasisiwa na Rais Dk. Samia yanayotujengea usawa, mshikamano na umoja kama taifa huru lililojengwa katika misingi ya demokrasia.

Rais hivi karibuni katika kutekeleza azma ya maridhiano aliyoyaanzisha ili kuvipa vyama vya siasa kutimiza haki yao ya kikatiba ameruhusu mikutano ya hadhara. CCM ni miongoni mwao vyama hivyo vya siasa ambavyo vimeruhusiwa kufanya mikutano ya hadhara jambo ambalo ni la kawaida kwa CCM.

Dhamira ya Rais Samia ni kujenga Tanzania katika misingi ya demokrasia usawa na kuheshimu haki za binadamu akiamini huu ndio msingi wa utawala bora, wakati anazungumza na wanasheria katika Jukwaa la Wanasheria wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anawaambia:

"Sisi Tanzania tumeamua kuizingatia misingi ya haki na nataka niwahakikishie kwamba tutajitahidi kuijenga iwe ya haki, demokrasia, usawa na mafanikio. Na ndio maana katika kipindi hiki nataka nisisitize kwamba kutenda haki na kuheshimu utawala bora ni misingi ambayo serikali yoyote inayotokana na watu hainabudi kuifuata bila shinikizo lolote kutoka nje. Kama serikali ni ya watu haina budi hiyo kufuata misingi hiyo."



Katibu wa Idara ya Uhamasishaji na Chipukizi UVCCM Taifa, Victoria Mwanziva.

> Ushauri wangu kwa vijana wenzangu wa CCM mtaji huu wa ukubwa na uwepo kila kona ya nchi hii usitufanye tubweteke tutafuteni taarifa sahihi tusome ilani na utekelezaji wake.

### UVCCM TUANZE

Mikutano hiyo ya hadhara ni fursa kwetu vijana wa CCM kwenda majukwaani kujenga hoja zenye mashiko kwa wananchi na kuwaeleza nini serikali yao inafanya chini ya Rais Dk. Samia, twendeni tukatengeneze ajenda za kujenga hima tusisubiri kujibu hoja au ajenda za wapinzani wetu.

Dunia kwa sasa imepiga hatua kubwa sana katika masuala ya teknolojia, matumizi ya mitandao ya kijamii imekuwa kwa kiasi kikubwa sana, katika ulingo wa siasa na uendeshaji wa serikali na upashaji wa habari huwezi kuikwepa mitandao ya kijamii. Wananchi wa kileo wengi wao wana uelewa mkubwa wa nini kinachofanyika katika nchi yao, vijana wengi ni wasomi wana ujuzi na matumizi ya mitandao ya kijamii.

Nawashauri twendeni kwenye mikutano ya hadhara tukijua hatuendi kuzungumza na Watanzania wa miaka 10 hadi 20 iliyopita, tujue tunaenda kuzungumza na kundi lenye taarifa ambazo zinaweza kuwa sahihi au sio sahihi. Hatuwezi kama vijana wa CCM kwenda kupambana majukwaani na vyama wapinzani wetu. Sisi mtaji wetu ni ilani ya uchaguzi 2020-2025 tuisome na tutafute taarifa sahihi za utekelezaji wake ili tupate hoja zenye mashiko na zenye ushawishi kwa wapiga kura wetu. Si kujibizana.

CCM imeandaa vizuri vijana na anaendelea kuwaandaa vijana wake katika siasa za hoja na ushindani katika demokrasia ya kweli. CCM ni chama chenye mfumo mzuri wa kupika vijana wenye uwezo wa kujenga hoja na kuyajua mambo mengi yanaenyoendelea katika taifa lao kwa undani, Chama Cha Mapinduzi kinaamini vijana ndiyo askari wa kukilinda chama, serikli na taifa ndani na nje.

### HATUJIBU WENZETU

Vijana lazima tusiwe watu wa kufukia mashimo yanayochimbwa na wapinzani bali tuwe wachimbaji na wao washindwe kuyafukia, lazima tuwe wasemaji wa kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia na Dk. Mwinyi katika taifa hilo. Ukubwa wa CCM siyo wa kujibu hoja za wapinzani bali ni kutenda, kuitekeleza ilani yake, kuwahudumia wananchi wake, jukumu la kuzungumza kukisemea chama na Rais wetu kwa wananchi ni kazi yetu vijana wa CCM.

CCM ipo kila mahali katika nchi hii ni chama kikubwa, ni taasisi iliyo imara yenye nguvu, ushawishi na ushupavu wa kiuongozi inayojitosheleza kila idara, mizizi ya CCM ni mirefu mikubwa na iliyokwenda mbali sana, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuna mahali hutaikuta CCM kwani inaongoza kwa kuwa na wanachama wengi katika taifa hili.

Tunao mtaji wa kutosha wa hoja kwani serikali ya CCM chini ya Dk. Samia imefanya mambo mengi awamu kwa awamu na hatua kwa hatua, kila eneo matakwa na mahitaji ya wananchi yanafanyiwa kazi na machache ambayo hayajafanyiwa kazi basi yapo kwenye mchakato wakufanyiwa kazi kwani serikali ya Rais Samia ni serikali sikivu.

Huu ni mtaji tosha wa vijana kwenda kujipambanua na kuzungumza yote yaliyofanyika, yanayofanyika na yanayotarajiwa kufanyika, hii itakuwa ni njia nzuri ya kuwapa wananchi taarifa sahihi na kufuta upotoshaji unaweza kuwafikia kupitia wanasiasa.

Ushauri wangu kwa vijana wenzangu wa CCM mtaji huu wa ukubwa na uwepo kila kona ya nchi hii usitufanye tubweteke tutafuteni taarifa sahihi tusome ilani na utekelezaji wake, tujue serikali yetu imetekeza nini kuwaeleza wananchi ukweli.

## Ni ishara kukubalika kitaifa, kimataifa, maridhiano, usawa kijinsia vyampaisha

INATOKA UK. 11

Kwa maana hiyo takriban Davos yote ni nyumbani kwake, iwe ni kwa wakuu wa nchi na serikali ambao wengi tu amefika kwao na wanamfahamu na hivyo wangemsikiliza au kwa wanaharakati na watetezi wa wanyonge, wanaotazamia apaze sauti.

Yako pia maeneo kadhaa ya uongozi wa Rais Samia au kufaulu kwake katika sehemu zinazoendana na mkutano wa Davos, kwa mfano matumizi ya fedha zinazotokana na jitihada za kusaidia Afrika kutatua mikwamo iliyotokana na wimbi la UVIKO-19 likafuatiwa na vita vya Urusi na Ukraine.

Hatua zilizochukuliwa ziliendana na jitihada zilizotangulia awali kwa mfano kuhakikisha kuwa mtoto wa kike anapata elimu kama wa kiume bila ubaguzi, na juhudi za kuinua kipato cha wanawake maskini na watu wenye mahitaji maalumu.

Aidha, alikuwa kiongozi wa kwanza wa Afrika kukaribishwa China baada ya mkutano mkuu wa chama tawala cha kikomunisti uliomthibitisha madarakani Rais Xi Jinping.

Ni wazi kuwa anakubalika kwa mataifa makubwa na anaendana na hisia za nchi nyingi za Afrika kuhusu China, Russia, uhusiano na Ulaya na Marekani, Dk. Samia anapatikana katika mwelekeo wake na kukubalika mambo mengi na ya aina tofauti ambayo si rahisi kuyakusanya kwa kiongozi mwingine.

# Dimwa awapa raha wana CCM, ahadi ya 90% ushindi 2025

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Muhammed Said Dimwa, akiwasalimia wanachama, waliokuwa pembezoni mwa barabara eneo la Michezani Mjini Unguja wakati wa mapokezi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

NAFASI ya Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, imeshashikiliwa na wanachama saba wa chama hicho tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992.

Kwa mara ya kwanza nafasi hiyo ilishikiliwa na Ali Ameir Muhammed, kuanzia mwaka 1992 hadi 1997. Na hivi karibu Halmashauri Kuu ya CCM, ikiongozwa na Mwenyekiti Taifa, Dk. Samia Suluhu Hassan, inamteua Dk. Said Muhammed Said au Dimwa, kushika jukumu hilo.

Dimwa anakuwa Naibu Katibu mkuu wa saba tangu mwaka 1992, akitanguliwa na wanachama sita waliobeba jukumu hilo, ambapo katika chaguzi zote kuu za nchi watangulizi wake hao walisimama kidete kuhakikisha chama hicho kinashika dola.

Mwaka 1998 hadi mwaka 2000 nafasi hiyo ilishikiliwa na Hassan Mussa Takrima na kijiti hicho kukabidhiwa Balozi Seif Ali Iddi hadi mwaka 2002 na yeye kumwachia Saleh Ramadhan Feruzi hadi ilipotimia 2011.

Vuai Ali Vuai, anaushika usukani kutoka kwa Feruzi mwaka 2011 hadi 2017 na yeye kumwachia Dk. Abdallah Juma Saadala, ambaye aliendesha gari la CCM hadi mwaka huu wa 2023.

Dk. Said Muhammed Said au Dimwa ni kiongozi kijana aliyezaliwa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ikilinganishwa na watangulizi wake na ndiye sasa mtendaji mkuu wa CCM visiwani hapa.

Matarajio ya wanachama wa CCM baada ya kupata kiongozi mpya huyo wa nafasi hiyo ya Naibu Katibu Mkuu ni kuendeleza umoja na mshikamano, demokrasia na kusogeza gurudumu mbele la maendeleo ili uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 chama hicho kiendelea kushika dola na kudumisha demokrasia.

Wana CCM wamempokea kwa furaha, shangwe na nderemo kiongozi huyo ambaye imani yao anaendana na kasi ya Mwenyekiti wa CCM, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu katika kuhakikisha chama hicho kinasonga mbele.

Bahati Issa mwana CCM na mkazi wa Kijiji cha Kikungwi Mkoa wa Kusini Unguja, anasema anatarajia kiongozi huyo mpya atatekeleza ilani ya CCM na chama hicho kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kwa kuwa kiongozi huyo ni kijana atakuwa na kasi ya kukiletea mabadiliko makubwa chama hicho na kuongeza idadi ya wanachama hodari na majasiri.

"Vijana ni nguvu kazi ya taifa hivyo sina mashaka katika utendaji wake wa kazi nina imani kuwa atalivusha salama jahazi la CCM Zanzibar kwa kushirikiana na viongozi wenzake akiwamo Makamu Mwenyekiti wa CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kulivusha salama jahazi hilo katika uchaguzi mkuu," anasema Bahati.

Simai Muhammed Said Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu pia ni Waziri wa Utalii anasema Dimwa amefanya kazi naye katika Baraza la Wawakilishi na wakiwa wajumbe wa Kamati ya Bajeti, akiwa mwenyekiti wao.

> "Namfahamu vizuri tulikuwa naye barazani ni kiongozi mwenye sifa na vigezo vinavyokwenda na wakati wa mabadiliko ya mahitaji ya siasa na demokrasia kwa sasa.

Anasema ni mchambuzi mahiri wa kuangalia hesabu na anayependa maoni kutoka kwa wajumbe wa kamati, na ilikuwa kamati yenye nguvu hasa pale wanapoibana serikali kutoa maelezo kuhusu matumizi ya fedha.

Anamsifia kuwa ni kiongozi mtaratibu, msikivu na hodari katika kusikiliza matatizo na kero za wananchi hivyo nafasi hiyo aliyoipata atakuwa karibu katika kukiongoza chama ili kushika hatamu.

"Dimwa ana uzoefu mzuri katika nafasi ya uongozi maana ameshashika nyadhifa mbalimbali ikiwamo uwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi wa Serikali ya Zanzibar, lakini ameshakuwa mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitia nafasi tano za wabunge Baraza la Wawakilishi, hivyo si mgeni katika masuala ya uongozi," anasema.

Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, anaeleza anavyomfahamu vizuri Dk. Dimwa kutokana na uwezo wake wa kujenga hoja katika mambo yenye maslahi kwa wananchi na kutaka serikali kuyasimamia haraka.

"Nilikuwa naye "bekbencha" ambapo ilikuwa tunajenga hoja zenye maslahi ya wananchi na kuitaka serikali kuzifanyia kazi haraka kwa maslahi ya wananchi wetu ambao ndiyo waliyotufikisha ndani ya Baraza la Wawakilishi,"anakumbusha.

Aidha, mwakilishi wa jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf, anasema anamfahamu mwakilishi Dimwa ambaye alipoingia katika barazani, alimsaidia kuibua hoja zinazowagusa wapiga kura katika jimbo langu na kuziwasilisha serikalini.

Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib anasema anamfahamu Dk. Dimwa ambaye anaamini ni chaguo sahihi kwa wakati muafaka katika kukiongoza chama cha mapinduzi kuelekea uchaguzi mkuu.

"Namfahamu vizuri tulikuwa naye barazani ni kiongozi mwenye sifa na vigezo vinavyokwenda na wakati wa mabadiliko ya mahitaji ya siasa na demokrasia kwa sasa," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa CCM, Khadija Jabir, anamtaka Naibu Dimwa asitoe mwanya wa kukaribisha majungu ambayo madhara yake makubwa ni kukigawa chama na wanachama wenyewe.

Aidha wanamwahidi kumpa ushirikiano mkubwa ambao ndiyo utakaofanikisha ushindi wa CCM kuelekea katika uchaguzi mkuu wa 2025.

"Sisi Baraza la Wazee wa CCM tunakupa baraka zote na tunakuahidi ushirikiano mkubwa ambao utakiwezesha chama kushinda katika uchaguzi mkuu ujao kwa kishindo kikubwa na ndiyo siri ya chama,"anasema.

Wenyeviti wa CCM katika mikoa sita ya kichama Zanzibar wanaahidi kufanya kazi kwa karibu na Naibu Katibu Mkuu Dimwa kutekeleza majukumu yake ya kukiongoza chama.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mberwa, anasema watahakikisha wanampa kila aina ya ushirikiano Naibu Katibu Mkuu mpya katika kuona chama kinafikia malengo ya ushindi na ujenzi wa demokrasia kama inavyoeleza ilani ya uchaguzi.

Akizungumza na wana CCM baada ya kupokelewa kwa shangwe visiwani Zanzibar kufuatia uteuzi huo, Naibu Katibu Mkuu Dimwa, anaahidi mengi ukiwamo ushindi wa kwa asilimia zaidi ya 90 katika uchaguzi mkuu wa 2025.

"Hakuna mkate mgumu mbele ya supu wenzangu aliyenitangulia amefanya kazi kubwa sana na CCM tukapata ushindi wa asilimia 76 mwaka 2020 lakini uchaguzi ujao tunataka kuvuka kiwango hicho kuhakikisha tunapata ushindi wa zaidi ya asilimia 90. Nia tunayo na malengo tunayo," anasema Dimwa na kuibua shangwe kwa wana CCM.

Anasema chini ya uongozi wake wanaandaa mpango kazi kuanzia ngazi za matawi, shina, jimbo, wilaya mpaka mkoa kwa kuweka mikakati ya kisiasa kuhakikisha CCM inasonga mbele.

Anakumbusha kuwa jambo la msingi kwa wanachama wa CCM ni kujenga umoja na mshikamano hasa kipindi hiki cha utekelezaji wa ilani ya chama huku akijiandaa na matayarisho ya uchaguzi mkuu wa 2025.

JUKWAA LA VIONGOZI

URUSI VS UKRAINE

# Putin amebakia kuwatumbua makamanda, vita ikimwelemea

**Na Mwandishi Wetu**

UNAPOKARIBIA mwaka mmoja wa vita vya Urusi dhidi ya Ukraine, mapambano yanaendelea tena yakiongeza hali ngumu kiuchumi duniani, kuanzia chakula, nishati na bidhaa za viwandani.

Kwa kifupi ni kama mambo ya mvamizi Urusi ni mabaya na safari hii Rais Vladimir Putin, anabadilisha tena viongozi wa vita akimteua Ofisa Mkuu wa Kijeshi, Valery Gerasimov kuwa msimamizi wa uvamizi wa nchi hiyo dhidi ya majirani zake Ukraine.

Ni katika kutumbua kulikofanyika karibuni tangu kuanza kwa vita. Amiri jeshi mkuu anamteua Gerasimov Mnadhimu Mkuu wa Jeshi kuimarisha vita vinavyodaiwa na nchi za Magharibi kuwa Urusi imeshindwa.

Miezi mitatu tu baada ya kufanya mabadiliko ya mara ya mwisho, Putin amemteua kamanda mwingine wa kuongoza kampeni ya Urusi nchini Ukraine, akionyesha kutoridhishwa kwa Kremlin na mwenendo wa kile kinachoitwa "operesheni maalum ya kijeshi" iliyozinduliwa Februari 24 mwaka jana.

Ofisa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, au mkuu wa wafanyakazi jeshini, amefanyakazi hiyo kwa muongo mmoja uliopita, katika mabadiliko yaliyomshusha cheo mtangulizi na bosi wake Sergei Surovikin, aliyetumbuliwa baada ya siku 95 za kufanyakazi ya kuongoza majeshi ya Urusi kuipiga Ukraine.


Mabadiliko hayo yanamaanisha kuwa sasa ni juu ya "mtu wa tatu muhimu zaidi katika uongozi wa kijeshi wa Urusi - baada ya Putin na Waziri wa Ulinzi Sergei Shoigu, kurekebisha hali ya Ukraine," anasema Jeff Hawn, mtaalamu wa jeshi la Urusi na mshauri wa Marekani katika kituo cha utafiti wa kijiografia na kisiasa cha New Lines.

Wanaomfuatilia nyendo zake wanasema ni mtu wa wastani kuliko 'Jenerali Armageddon'

Valery Gerasimov (67), sio tu ofisa wa cheo cha juu zaidi katika jeshi; yeye pia ni aina tofauti sana ya kamanda kutoka kwa Sergei Surovikin, ambaye aliitwa "Jenerali Har-Magedoni" kwa sababu ya ukatili na ubakaji.

Akiwa mkuu wa muda mrefu zaidi wa wafanyakazi au Mnadhimu Mkuu tangu nyakati za Soviet, Gerasimov, anaweza kujivunia mafanikio yakiwamo ya zamani huko Chechnya na Crimea. "Pia anaonekana kama ana ushawishi wa kudhibiti mambo kuhusu vita na ni mtu ambaye Washington inaweza kufanya kazi naye," anasema Hawn.

"Yeye si 'Jenerali Har-Magedoni' kama Surovikin aliyetumbuliwa, kwa hakika, lakini haijulikani wazi ni kiasi gani cha matokeo anayoweza kuleta kwenye vita na hasa wakati huu wa mapigano," aonya Stephen Hall, mtaalamu wa Urusi katika Chuo Kikuu cha Bath.



Rais wa Urusi, Vladimir Putin, akiwa na generali aliyemtumbua Ukraine, Sergey Surovikin. **PICHA ZOTE: REUTERS**

> Valery Gerasimov (67), sio tu ofisa wa cheo cha juu zaidi katika jeshi; yeye pia ni aina tofauti sana ya kamanda kutoka kwa Sergei Surovikin, ambaye aliitwa 'Jenerali Har-Magedoni' kwa sababu ya ukatili na ubakaji.



Generali Valery Gerasimov, kamanda mpya wa vita vya Ukraine.

Anaongeza kwa hakika, "hata kama angetaka kurekebisha mfumo wa uendeshaji wa jeshi la Urusi, hatakuwa na vifaa, wala njia, wala wafanyakazi wa kufanya hivyo wala mbinu mpya," anaongeza Hawn.

Kwa mtazamo wa kijeshi, mabadiliko au kutumbua huko ni "uthibitisho kuwa ulihitajika na kwamba kutakuwa na mambo mabaya siku zijazo na kwamba hata Putin anatambua kuwa uratibu mbaya wa shughuli za kivita umekuwa tatizo na ndilo suala lililochangia kuboronga," mchambuzi wa usalama wa Urusi Mark Galeotti, anaandika kwenye mtandao wa twita.

Kwa hivyo mambo haya yanamaanisha nini? Mosi ni uthibitisho, ikiwa tuliuhitaji muongozo mwingine au kwamba kutakuwa na mambo makubwa mabaya yanayokuja na kwamba hata Putin anatambua kwamba uratibu mbaya wa mambo umekuwa chanzo cha kuchemka huko Ukraine. Ingawa hata Gerasimov anapoingia sasa anaweza kuamrisha vikosi vya jeshi na kundi la mamluki kuwaamrisha mamluki Wagner na jeshi la Kadyrovtsy, kweli? Ndiyo ujumbe wa twita.

Katika taarifa iliyotangaza kuteuliwa kwa Gerasimov, ikitolewa na Wizara ya Ulinzi ya Urusi inasema lengo ni "kuandaa uratibu na kufanyakazi kwa karibu kati ya matawi ya jeshi". Majukumu yake hayo pacha kama Mnadhimu wa Jeshi na Kamanda Mkuu nchini Ukraine yanamaanisha kuwa ana zana zote mkononi za kutekeleza jukumu hilo na anatarajiwa kuwa ataweza kuwasilisha mbinu mpya angalau kwa kuandika kwenye karatasi.

Kumtoa Gerasimov kafara au kudhoofisha maluki ya Wagner? Ni swali ambalo wachambuzi wanahoji? Umuhimu wa kutumbua hata hivyo, unaweza kuwa wa kisiasa, ukifika wakati wa mabadiliko katika vita vya kiushawishi kati ya jeshi la Urusi na kikundi cha mamluki cha Wagner kinachoongozwa na mfanyabiashara bilionea Yevgeny Prigozhin.

Hali ya Jeshi la Urusi imeonekana kuwa taabani, na uthabiti na uwezo wake umeporomoka vibaya baada ya msururu wa vikwazo nchini Ukraine lakini shambulio baya la mwaka mpya la makombora mazito kwenye kambi ya Warusi huko Makiivka, ambalo lilibainisha uzembe na kukosekana weledi wa viongozi wakuu wa kijeshi.

Cha kushangaza wakati kambi ikilipuliwa bilionea Prigozhin na mamluki wake wa Wagner wamekuwa wakitunishiana misuli kuzungumzia vita vikali huko Soledar, vikipiganwa mapema mwaka huu wakidai waliwashinda walishinda na kuuteka mji wa Donbas wa Ukraine pekee. Wakiwa wamekasirishwa na maneno ya Wagner, Jeshi la Urusi liliwahi kuelezea kwamba mapigano bado yalikuwa yanaendelea na kwamba askari wake wa miavuli walihusika sana katika vita hivyo vya Donbas.

Wakati matokeo ya umwagaji damu huko Soledar bado hayajulikani, Kundi la Wagner tayari limeshinda vita vya kujigamba na kujiimarisha maoni huko Moscow kwamba wanamgambo wa hao mamluki wa Prigozhin wako mstari wa mbele katika vita vya Urusi katika miezi kadhaa. Hivyo kupewa 'sapoti' zaidi na wakosoaji wa kitaifa wa kijeshi na kumruhusu bilionea Prigozhin anayewasimamia mamluki hao kupata sifa zaidi ya mpinzani wake huko Kremlin, Waziri wa Ulinzi Shoigu.

Kwa kuzingatia mabadiliko hayo uteuzi wa Gerasimov ni "kuona kama onyo lililotolewa na Putin kwa Prigozhin wa kundi la Wagner, kwa hivyo hafikirii kuwa anaweza kufanya chochote anachopenda", anasema Hall.

Akiwa mmoja wa washirika wa karibu wa Waziri wa Ulinzi Shoigu, kamanda mkuu mpya inamaanisha uwezekano wa kulinyima uhuru kundi la Wagner au kulipa uhuru kidogo zaidi kuliko mtangulizi wake Surovikin, ambaye anachukuliwa kuwa karibu kiitikadi na bilionea Prigozhin hivyo kuwabeba mamluki.

Hata hivyo kuanzia sasa na kuendelea, Kamanda Mkuu Valery Gerasimov, yuko kwenye mstari wa kutumbuliwa na hawezi tena kuwalaumu wengine iwapo hali itazidi kuzorota nchini Ukraine inaonekana kama amewekwa katika hali ya kukwama, ambayo itampa Putin kisingizio cha kumwondoa jeshini kwa ulaini iwapo hali itaendelea kuzorota zaidi kwenye vita vya Ukraine.

**CHANZO FRANCE 24**





## 'Wadau wanaoendesha mashauri ya watoto wanahitaji mafunzo endelevu'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHUO cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kimefanya utafiti na kubaini kuwa wadau wanaoendesha mashauri ya watoto wanahitaji kupata fursa za mafunzo endelevu ili kwenda na wakati katika kufanya uamuzi wa mashauri hayo.

Akizungumza jana jijini hapo katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini, Mhadhiri Msaidizi wa Chuo hicho, Roggea Ndyanabo, alisema baada ya utafiti huo chuo kilitoa fursa ya kozi endelevu kwa wanaohusika katika mashauri hayo.

Alisema waendesha mashauri hao wanahitaji elimu endelevu ili kuhakikisha wanatoa haki kwa watoto.

"Utafiti wetu ulibaini waendesha mashtaka ya watoto wanahitaji elimu hivyo serikali inapaswa kuwaendeleza," alisema Ndyanabo.

Aidha, alisema, wamefanya utafiti wa migogoro ya ardhi na kuangalia namna ya kuisuluhisha nje ya mahakama suala ambalo alisema litaokoa gharama na muda wa wananchi na kuwawezesha kufanya shughuli za maendeleo badala ya kutumia muda mwingi mahakamani kufuatilia kesi za migogoro hiyo.

Alisema migogoro ya ardhi, masuala ya mirathi yamekuwa changamoto katika jamii na yanapaswa kufanyiwa kazi.

Kadhalika, chuo hicho kinatoa mafunzo kwa ngazi mbalimbali zikiwamo kozi fupi na ndefu.

"Kozi ndefu tunatoa astashahada ya sheria na stahahada ya sheria na kozi fupi tunatoa kwa watumishi wa mahakama kwa ujumla.

Ndyanabo aliwaasa wananchi watembelee banda lao ili kujifunza zaidi shughuli zinazofanywa na chuo hicho.

Alisema watapata elimu kuhusu chuo hicho kazi inazofanya pamoja na msaada wa kisheria katika mambo mbalimbali nchini.

# Vijana kuendelea kujengewa uwezo kujikwamua kiuchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali itaendelea kutoa kipaumbele na kuweka mikakati mbalimbali ya kuwajengea vijana mazingira wezeshi ili kujikwamua kiuchumi.

Katambi aliyasema hayo juzi jijini hapo kwenye hafla ya kuwakaribisha wanafunzi wapya wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa mwaka wa masomo 2022/23.

Alisema dhamira ya serikali ni kuwapatia vijana elimu bora na thabiti inayoendana na mazingira yao na kuhakikisha elimu hiyo inawasaidia katika kuhudumia taifa na kuwapatia maarifa ili kujiongoza.

"Vijana ndiyo nguvu kazi ya taifa na serikali ina matarajio makubwa na kundi hilo kwa kuwa ndio watakaoleta mapinduzi ya ukuaji wa uchumi wa nchi," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuweka mikakati endelevu yenye malengo ya kuwezesha vijana ikiwamo kuwapatia mikopo yenye riba nafuu ambayo hutolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Vilevile, mikopo inayotolewa na halmashauri mbalimbali zilizoko nchini kupitia mapato ya ndani ambayo imewezesha vijana kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali inayowaingizia kipato.

Alitaja jitihada nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuwezesha vijana kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi na kupitia mafunzo tarajari (Internship) yanayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Kitengo cha Huduma za Ajira (TaESA) imewezesha wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kushiriki mafunzo ya uzoefu wa kazi na baadhi ya vijana wameajiriwa na kampuni mbalimbali.

Pia kitengo hicho kimewaunganisha vijana na fursa za ajira nje ya nchi ikiwamo wakati wa kombe la dunia na miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa nchini.

Aliwataka vijana hao kutambua wajibu walionao na kuwa na tabia njema ili kufanikiwa na kutimiza malengo yao.

Naye Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Prof. Hosen Mayaya, alishukuru serikali kwa kuendelea kuwezesha sekta ya elimu nchini ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika kukomboa taifa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki (kulia), akikabidhi hati ya utunzaji mazingira ya bustani iliyoko eneo la Medeli jijini Dodoma kwa Meneja Mauzo wa Vodacom Mkoa wa Dodoma, Balikulije Mchome, wakati wa mkutano wa kuutangazia umma mafanikio ya mkoa humo na serikali. Vodacom iliomba kupewa na kuligeuza eneo la Medeli kuwa bustani kupitia kampeni yake ya Kijanisha Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMISEMI kuipa nguvu Bodi ya Mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeanza kufanya marekebisho na maboresho ya muundo wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ili kuipa nguvu na uwezo wa kutoa mikopo yenye tija na kufuatilia marejesho.

Naibu Waziri wa ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyokuwa ikipokea na kujadili taarifa ya utendaji wa bodi hiyo na taarifa ya utendaji wa Shirika la Masoko ya Kariakoo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

"Ni kweli Bodi ya Mikopo imekuwa na sheria za zamani, kwa hiyo tunaboresha sheria na kanuni kwa kuweka miongozo itakayosaidia Bodi ya Mikopo kuwa na uwezo wa kutoa mikopo na kufuatilia marejesho," alieleza.

Dk. Dugange alisema bodi hiyo itaongezewa nguvu ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kusaidia halmashauri kunufaika na mikopo.

Alisema moja ya jukumu la msingi la bodi hiyo ni kuzikopesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa madhumuni ya kutekeleza miradi iliyolenga kuziongezea mapato, kuchochea shughuli za kiuchumi, kuongeza ajira na kuboresha utoaji wa huduma.

Kuhusu utendaji wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, Dk. Dudange alisema TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala Mikoa kuhusu utaratibu na viwango vya kufuata wakati wa kujenga masoko ili kuepuka na kupambana na majanga ya moto.

Pia alisema ili kuimarisha usafi katika masoko, serikali ipo mbioni kuanza utaratibu wa kubadilisha taka ngumu kuwa nishati mbadala na mpango huo unaendelea kufanyiwa utafiti.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jaffari Chaurembo, alisema maboresho ya muundo wa bodi hiyo yatasaidia halmashauri kunufaika na kuipa uwezo kufuatilia marejesho.



# Maofisa kilimo kuwa na mavazi maalumu ya kuwatambulisha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imesema itawaandalia mavazi maalumu maofisa kilimo wote wa ngazi za vijiji na kata nchini ili yawatambulishe kwa wakulima mahali popote watakapokuwa wanapita kuwahudumia.

Aidha, imesema itawaandalia maofisa hao pikipiki maalumu watakazozitumia kwenda kuwahudumia wakulima mashambani na kufika kwa wakati kuwafundisha mbinu za kilimo bora cha mazao mbalimbali.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, aliyasema hayo wilayani Mbarali, alipotembelea miradi mbalimbali ya umwagiliaji likiwamo bwawa la Rwanyo ambalo ujenzi wake unatarajiwa kuanza upya baada ya kukwama kwa zaidi ya miaka 10.

Mavunde alisema lengo la kuwaandalia vifaa hivyo ni kuwatambulisha kwa wakulima na kuhakikisha wanafika kwenye maeneo yao ya kazi kwa wakati ili kuongeza uzalishaji wa mazao yanayozalishwa kwenye maeneo yao.

Alisema wakulima wakimwona ofisa huyo mahali popote akiwa amevaa mavazi hayo watakuwa huru kuwaita na kuwaeleza kero zinazowakabili kwenye mashamba yao ili waende wakawasaidie.

"Lakini pikipiki watakazopewa tutazifunga mfumo maalumu ambao utakuwa unasaidia kuhakikisha wanazitumia kwa kazi iliyokusudiwa, akitoka eneo lake la kazi pikipiki itazimika mara moja mpaka atoe maelezo ya kujitosheleza," alisema Mavunde.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha uzalishaji wa mazao mbalimbali unaongezeka kwa kiwango kikubwa ili taifa lijitosheleze kwa chakula na ziada iuzwe nje ya nchi na kuliongezea taifa pato.

Aliwataka maofisa kilimo wa wilaya zote nchini kuwasimamia vizuri maofisa hao ili kuongeza tija kwenye uzalishaji na kufikia malengo mbalimbali ya serikali ikiwamo Agenda 2030 ambayo inalenga sekta ya kilimo kuwa miongoni mwa zinazochangia ukuaji wa pato la taifa.

Baadhi ya wakulima wa Wilaya ya Mbarali walisema utaratibu huo unaotarajiwa kuanzishwa na serikali, utawasaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao yao.

Mmoja wa wakulima hao, Jeremiah Sanga, alisema katika wilaya hiyo ni maeneo machache maofisa kilimo wanaonekana mengine wanazalisha kwa kutumia mbinu zao za asili ambazo hazina tija.

Alisema Wilaya ya Mbarali wananchi walizalisha zaidi mpunga kuliko mazao mengine, lakini wakulima wengi wanalima kilimo cha mazoea ambacho ni kwa ajili ya kupata chakula.

"Maofisa kilimo wapo kwenye mashamba makubwa ya wawekezaji, ndiyo maana uzalishaji wa kampuni na sisi wakulima wadogo hauendani, wenzetu ambao wapo jirani na mashamba ya wawekezaji wanazalisha vizuri maana wao wananufaika na mbinu za kwenye kampuni," alisema Sanga.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema uchumi wa wilaya hiyo unategemea zaidi kilimo cha mpunga ambalo ndilo zao linalozalishwa kwa wingi zaidi ikilinganishwa na mazao mengine.

Alisema msimu uliopita wilaya hiyo ilizalisha tani 460,000 za mpunga, lakini mahitaji ya chakula ni tani 120,000 pekee, kiasi kilichobaki ni kwa ajili ya biashara.

Vilevile, alisema asilimia kubwa ya viwanda vilivyoko katika wilaya hiyo ni vya kuchakata mpunga.



Taka zikiwa zimetelekezwa bila ya kuzolewa juu ya chemba ya majitaka kando ya barabara ya kuingia katika Shule ya Msingi Ikulu, Kata ya Ilomba jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Miche 900,000 ya vanilla yasambazwa kuhamasisha

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, imesambaza zaidi ya miche 900,000 ya vanila kwa wakulima 1,200 wa maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kuhamasisha kilimo cha mkataba cha zao hilo ambalo lina soko kubwa duniani.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Rungwe, Juma Mzara, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu maendeleo ya kilimo cha zao hilo na kusambaza miche hiyo kwenye kata zote zinazozalisha zao hilo.

Alisema zao hilo ni miongoni mwa yasiyoathirika kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi na halihitaji maji mengi kama ilivyo mengine.

Alisema miche hiyo imezalishwa na wadau mbalimbali wa zao hilo ambao waliwezesha uandaaji wa mitalu vya kuzalishia miche hiyo kitaalamu na kuzisambaza kwa wakulima.

"Miche hiyo iliyosambazwa kwa wakulima kwa sasa baadhi imeanza kutoa matunda na wanatarajia kuanza kuvuna mwakani, wapo ambao waliwahi kuingia kwenye kilimo hiki sasa hivi matunda yapo," alisema Mzara.

Alisema kwa sasa wanakabiliwa na tatizo la elimu ndogo kwa wakulima kuhusu kilimo cha vanila na akawataka maofisa kilimo wa maeneo yote ya wilaya hiyo kuwaelimisha wananchi.

Baadhi ya wakulima walioanza uzalishaji wa zao hilo wameishukuru serikali kwa kuweka mazingira rafiki ya wakulima kuzalisha mazao ya tofauti ili kuimarisha uchumi.

Mmoja wa wakulima hao, Mboka Mwakatumbula, alisema kuwa ujio wa kilimo cha vanilla umeongeza idadi ya mazao ya biashara katika wilaya hiyo tofauti na yale yaliyokuwa yanazalishwa awali.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alihamasisha wananchi hususan wakulima kuongeza tija uzalishaji wa mazao ya kimkakati ambayo yanastahimili ukame ili kuimarisha kipato kwa wananchi.

# Wakazi Ikombe wafurahia neema nishati ya umeme

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAKAZI wa Kijiji cha Ikombe, Kata ya Matema kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa wilayani Kyela, wameanza kunufaika na nishati ya umeme kwa kuitumia kuhifadhi samaki kabla ya kupeleka sokoni kuuza.

Kijiji hicho kiliwashiwa nishati hiyo juzi ikiwa ni mara ya kwanza tangu nchi ilipopata uhuru jambo ambalo lilikuwa linasababisha washindwe kuhifadhi baadhi ya vitu vyao kwa muda mrefu wakiwamo samaki.

Umeme huo uliwashwa na maofisa wa Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA), baada ya mradi wa ujazilizi wa nishati hiyo kukamilika katika kijiji hicho.

Diwani wa Kata ya Matema, Anthony Mwamgunda, alisema baada ya kijiji hicho kuunganishiwa umeme, wananchi watanunua majokofu kwa ajili ya kuhifadhi samaki wanaovuliwa ziwani ili wakae muda mrefu bila kuharibika.

Alisema hali hiyo itasaidia kuboresha soko la samaki na kuongeza pato la wananchi mmoja mmoja, halmashauri ya Kyela pamoja na taifa kwa ujumla kwa kukusanya fedha zitokanazo na ushuru.

"Fedha hizo ndizo zitaletwa tena kwa wananchi wangu kuja kujenga barabara, vituo vya afya, shule na miundombinu mingine muhimu, kwahiyo tunaishukuru serikali kwa kutuletea nishati hii muhimu," alisema Mwamgunda.

Christina Konala, mkazi wa kijiji hicho, alisema utaratibu wa serikali kusambaza umeme vijijini utasaidia kupunguza vitendo vya vijana kuhama vijijini na kukimbilia maeneo ya mjini ambako huduma zote muhimu zinapatikana.

Alisema umeme utawafanya vijana kuanzisha shughuli mbalimbali za uzalishaji zinazohitaji nishati hiyo ikiwamo uchomeleaji, vinyozi na hata maduka ya vinywaji baridi.

"Watu watakuwa wanahifadhi vitu kwenye mafriji ili vikae muda mrefu kama wenzetu wa mjini wanavyoishi, tutapata maendeleo kama ilivyo maeneo mengine," alisema Christina.

Meneja wa Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) wa Wilaya ya Kyela, Mhandisi Mustapha Himba, alisema vijiji katika wilaya hiyo ambavyo vilikuwa havijaunganishiwa nishati hiyo vilikuwa 35, lakini baada ya mradi huo kukamilika vitapungua.

Alisema kwa sasa mradi huo umetekelezwa katika vijiji 16 ambavyo kabla vilikuwa havina umeme huku akieleza kuwa wamefunga transfoma 10 zitakazohudumia vijiji hivyo.

Alisema katika maeneo yaliyobaki wanaendelea na upembuzi ili wakamilishe kabla ya kuhamia kwenye vijiji vingine vilivyo kwenye mpango.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Ismail Mlawa, aliwataka wananchi kulinda miundombinu ya umeme inayojengwa kwenye maeneo yao ili idumu.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi kujenga miundombinu hiyo na mwananchi lazima wailinde kutokana na fedha zinazotumika zinatokana na kodi zao wenyewe.



# Wenye ulemavu hatarini kukosa haki za msingi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAHARAKATI wa kutetea haki za wanawake na watoto wamesema kuwa makundi yalio pembezoni yakiwamo ya watu wenye ulemavu yapo katika tishio la kukosa haki za msingi ikiwamo elimu na kukabiliwa na matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

Akizungumza jana katika mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari jinsi ya kuibua changamoto zinazowakabili makundi hayo ya pembezoni, Mwanaharakati Asha Aboud Talib, alisema wanawake na watoto ni waathirika wakubwa wanaokoseshwa haki zao za msingi na wanakabiliwa na wimbi kubwa la ukatili na udhalilishaji.

Mwanaharakati huyo aliwataka waandishi wa habari kuziibua changamoto wazokabiliana nazo makundi hayo ikiwamo watu wenye ulemavu na kurudisha nyuma juhudi zao za maendeleo.

Alisema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha juhudi zao za kupata maendeleo ikiwamo ukosefu wa kupata mitaji ya fedha kwa ajili ya kuendesha biashara kwa sababu wengi wao hawakopesheki kutokana na uwezo mdogo walionao.

Alisema zipo taasisi za fedha ambazo zinatoa fedha za mikopo kwa makundi mbalimbali kuendesha shughuli za ujasiriamali, lakini kwa makundi ya watu wenye ulemavu hadi sasa hayajafikiwa vizuri.

Kwa upande wa sekta ya elimu, alisema bado hakuna miundombinu rafiki inayowawezesha watu wenye ulemavu kupata fursa ya elimu kama wenzao ikiwamo ukosefu wa vifaa vya kufundishia na majengo ya shule sio rafiki.

"Wizara ya Elimu hadi sasa wanajenga majengo ya shule ikiwamo ya ghorofa, lakini kwa bahati mbaya hakuna miundombinu rafiki itakayowawezesha kundi hilo kupata haki na fursa za elimu sawa," alisema.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Dk. Sikujuwa Hamdani, aliwataka waandishi wa habari kuzifahamu baadhi ya sheria ambazo bado zinakabiliwa na changamoto mbalimbali na kurudisha nyuma juhudi za maendeleo kwa kundi la wanawake na watoto kiasi ya kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia.

Alizitaja baadhi ya sheria zinazohitaji kufanyiwa marekebisho ikiwamo Sheria ya Mahakama ya Kadhi Zanzibar ambayo licha ya kufanyiwa marekebisho mara mbili katika kipindi cha mwaka mmoja, baadhi ya kasoro ni kikwazo katika kuimarisha ustawi wa wanawake na watoto kuyafikia malengo yao.

Alisema sheria hiyo inamkosesha mwanamke kupata haki zake baada ya kuachana na mwenza wake kwa kushindwa kupata stahiki zake ikiwamo mgawo wa mali walizochuma pamoja katika kipindi cha ndoa yao.

"Suala la mgawo wa mali waliochuma wanandoa baada ya kuachana katika sheria ya mahakama ya kadhi bado ni changamoto kubwa na ndiyo maana upo umuhimu mkubwa kwa kuwapo kwa sheria moja itakayoshughulikia mambo yote ya Waislamu," alisema.

Baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki mafunzo hayo walisema wakati umefika kuwapo kwa sheria moja itakayoshughulikia moja kwa moja masuala yote yanayowahusu Waislamu katika masuala yanayowahusu tofauti na sasa kuna sheria nyingi zinazohusu jamii hiyo, lakini hazijakamilika.

"Wakati umefika tukawa na sheria moja inayohusu mambo ya Waislamu ikiwamo talaka, mgawanyo wa mali pamoja na matunzo ya watoto na mirathi tofauti na sasa zipo sheria nyingi ambazo hazijakamilika," alisema Said Salim Said, mwandishi wa habari mwandamizi.

Alisema wanawake ndiyo waathirika wakubwa katika Sheria ya Mahakama ya Kadhi ambayo kwa kiasi kikubwa katika mfumo wa muundo wake inaendeshwa na wanaume pekee kuanzia majaji hadi mahakimu wake pamoja na Baraza la Maulama kiasi cha wanawake kupoteza imani kwa mahakama hiyo katika kupata haki zao.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), ofisi ya Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema elimu inahitajika kwa jamii kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambavyo kwa sasa vimeshamiri visiwani humo.

Aliwataka waandishi wa habari kupaza sauti zao kupitia taaluma yao kupambana na vitendo hivyo kwa sababu matukio yanayoripotiwa ni mengi, lakini hukumu ni chache.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu masuala ya udhalilishaji yaliofanyika katika ofisi za TAMWA Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Maeneo sita yaainishwa kujengwa mji wa serikali

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Dk. Mngereza Mzee Miraji, amesema wizara hiyo imeshakamilisha ramani ya mji wa serikali kiutendaji kwa awamu ya kwanza na maeneo sita yameshaainishwa kwa ajili ya kujenga mji huo.

Akizungumza baada ya kumaliza kikao baina ya wizara hiyo na Taasisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB), kilichofanyika mwisho wa wiki Kiembesamaki Unguja, alisema ramani ya Mji wa Serikali imekamilika na muda mfupi serikali itaamua wapi ujengwe mji huo.

Dk. Mngereza aliyataja baadhi ya maeneo yaliyopendekezwa kuwa ni Fumba, Kisakasaka, Dunga na Tunguu na yameonekana yanafaa kutokana na vigezo vinavyohitajika katika Mji wa Serikali.

"Ni kweli mwezi mmoja uliopita tuliwaita watendaji wa wizara zote za serikali wizarani watupe maoni yao ya mwisho ili tukafanye marekebisho katika dizaini (design) ya Mji wa Serikali iliyokuwapo, lakini leo maeneo yaliyoainishwa ni Fumba, Kisakasaka, Dunga na Tunguu," alisema Dk. Mngereza.

Alisema chanzo cha fedha za ujenzi wa mji huo hakijafahamika, lakini serikali ikishaamua kujenga sehemu bila shaka kutakuwa na chanzo cha fedha na bajeti yake.

Pia alisema kupitia kikao hicho wamekubaliana majukumu baina Wizara ya Ardhi na Taasisi ya PDB kukamilika kwa kipindi cha muda wa wiki moja.

Mkurungenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba (ZHC), Mwanaisha Ali Said, alisema kikao hicho ni muhimu kwa sababu ZHC ina changamoto ya kiutendaji ikiwamo fedha, jinsi ya kupata na kuandika maandiko ya kuzipata na vipaumbele mbalimbali.

"PDB ni taasisi muhimu kwa ZHC kwa kutumia utaalamu wao katika sekta ya nyumba na ya uendeshaji miradi, wametusaidia kutuongoza kwa kuwa vipaumbele vya mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni vingi hata vipaumbele vya Shirika la Nyumba Zanzibar pia ni vingi," alisema Mwanaisha.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasilino na Habari kutoka Taasisi ya PDB, Dk. Mohamed Mansour Nassor, alisema taasisi yake inajua Shirika la Nyumba Zanzibar namna gani linavyofanya kazi, mikakati yake, mafanikio pamoja na changamoto.

# Madaktari wanyama watakiwa kuepusha vifo vya mifugo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MADAKTARI wa Idara ya Mifugo wametakiwa kuongeza jitihada katika kazi zao ili kuepusha vifo vya wanyama wanapopata maradhi na kuongeza ufanisi kwenye sekta ya mifugo.

Akizungumza jana baada ya kukabidhi vifaa vya maabara ya uchunguzi wa wanyama katika ofisi ya maabara hiyo Maruhubi Zanzibar, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema vifaa hivyo vitumike kwa lengo lililokusudiwa ili kuleta ufanisi katika kutambua mashambulizi ya magonjwa hatari yanayowapata wanyama.

Shamata alisema itafurahisha kuona vifaa hivyo vinatumika kwa uangalifu na kuwasaidia madaktari kuchunguza wanyama waliokufa na kubaini chanzo cha vifo vyao.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Seif Shaaban Mwinyi, aliwataka madaktari hao kuvitunza vifaa hivyo ili kudumu sambamba na kulinda afya ya binadamu na wanyama kuepusha maradhi yanayotokana na wanyama.

"Kuna wakati vyanzo vya vifo vya binadamu hutokana na mifugo hivyo niwaombe madaktari mjitahidi kuweka usalama wa mifugo ili wawe na afya nzuri na kuepukana na maradhi," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya watendaji wenzake, Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Asha Mohamed Zahran, alisema vifaa hivyo vitawezesha kufuatilia kwa karibu afya za mifugo na kuchunguza sababu ya vifo ili kudhibiti maradhi nchini.

Aidha, vifaa hivyo vitaondoa changamoto zinazoikabili maabara hiyo na kuwaomba wafugaji kuacha kutumia dawa kiholela kwa kufuata taratibu wanazopangiwa na madaktari wa mifugo.

Mtaalamu wa maabara wa wizara hiyo, Fatma Waziri, aliishukuru wizara kwa kuwapatia vifaa hivyo vitakavyosaidia kuondoa changamoto za wafugaji na kuwahamasisha madaktari walioko wilayani kupeleka sampuli katika maabara kwa ajili ya uchunguzi wa maradhi yanayowakabili mifugo.

Vifaa hivyo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo vya maabara na vifaa vya uchunguzi wa awali vya kuchunguza wanyama waliokufa vilivyokabidhiwa vina thamani ya shilingi milioni 19.4 na vimetolewa na wizara hiyo kwa ufadhili wa Shirika la Chakula Duniani (FAO).

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1135 OF 2022
In the Matter of the Estate of the Late
JOHN BUSHIA NKINGWA
and
In the Matter of Application for Letters of Administration by
JOSEPHAT JOHN NKINGWA

**GENERAL CITATION**
(Rule 75)

**All persons** claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 07 day of February, 2023.
Dated at DAR ES SALAAM this 08 day of December, 2022.

Senior Resident Magistrate

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM
Usimamizi wa mirathi Na. 81 / 2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU ADAM BAKARI MTAKA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA
MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA
BAKARI ADAM BAKARI

**TANGAZO**
*(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 02 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 19 mwezi 01 mwaka 2023

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASHA KIBIRA HANGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 449 CMD TOYOTA – RAV 4.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/33146/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SIABA J. KAYANGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 624 DKC.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **IR/IRI/RB/31560/2023.**

---

MAHAKAMA YA TANZANIA
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
ILIYOPO SHINYANGA
SHAURI LA MAMLAKA YA ZIADA
SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NAMBA 6 YA 2022
- MAXIE SONDO……MDAI
- JOHN BUTONDO
- BLANDINA GOGADI

DHIDI YA
- BARAKA MIGERA
- HAMPHLEI KIMARO……WADAIWA

**KWA: HAMPHLEI KIMARO**
**POPOTE ULIPO**

**TANGAZO**
UNAJULISHWA KUHUDHURIA KATIKA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 26/01/2023 SAA 3:00 ASUBUHI KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI SHINYANGA.
HIVYO UNAAMRIWA KUHUDHURIA SIKU HIYO BILA KUKOSA NA KAMA HUTAHUDHURIA KESI HIYO ITASIKILIZWA NA KUTOLEWA UAMUZI BILA WEWE KUWEPO.
HATI HII IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 12/12/2022

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
SHINYANGA

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MOROGORO
MKOA WA MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na……11/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: ALLY IBRAHIMU SULEMAN WA BUNDI STREET
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA SHAZMA ALLY IBRAHIM

**TANGAZO**
*(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27 Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 01 mwaka 2023

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TEMAELY BRAYSON MSENGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 203 BYD** na **CHASSIS NAMBA: KE7KEFPK034398.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/33516/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARLIN LEONCE KOMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T239AQW** aina ya Toyota Camry yenye Chassis **No. SV400139331, Engine No. 451427819.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/473116/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHRISTOPHER STEPHEN HIZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T739BAS** aina ya **NADIA,** yenye **Chasis No. SXN100048428.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/473120/2022.**

---

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

---

# BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD

WE ARE DEALING GENERAL AUCTIONING, DEBT COLLECTION, EVICTION, INVESTIGATION AND REPOSSESSION, STORAGE, COMMISSION AGENCY AND GENERAL BUSINESS.

## NOTICE OF SALE AND INVITATION OF SEALED BIDS FOR SALE OF PROPERTY

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** under the powers contained in the law and Mortgage Deed and other powers enabling us to do so, We **BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD** of **P.O.BOX 16095** , Dar es Salaam, duly appointed by **BANK OF AFRICA (T) LTD** to sell the mortgaged property "as they are" by sealed bids. **WE HEREBY INVITE BIDS FROM GENERAL PUBLIC** for the outright purchase of the properties described in the table below

| S.N | PROPERTY DESCRIPTION | LOCATION | Property Registration Owner | Bids Submission deadline Date | Bids Opening Date |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Property held under derivative right on CT no. 12087,MBYLR,plot no. 33 block "M" | MIYOMBONI IN IRINGA MUNICIPALITY | **EDDIE HANS POPPE,ZACHARIA HANS POPPE AND CAESAR HANS POPPE** | On 08TH February 2023 before 08;30AM hours at the address below | On 08TH February 2023 before 09;00AM hours at the address below |
| 2 | Property held under derivative right on CT no. 6406,MBYLR,plot no. 68 & 69 block "M" | MIYOMBONI IN IRINGA MUNICIPALITY | **ZACHARIA HANS POPPE,HARRY HANS POPPE,EDDIE HANS POPPE,CAESAR HANS POPPE AND ALDO HANS POPPE** | On 08TH February 2023 before 08;30AM hours at the address below | On 08TH February 2023 before 09;00AM hours at the address below |
| 3 | Property held under derivative right on House no. 10, Plot no. 1057 block "L" | MBEZI BEACH AREA IN DAR ES SALAAM | **Z. H. POPPE LTD** | On 08TH February 2023 before 08;30AM hours at the address below | On 08TH February 2023 before 09;00AM hours at the address below |

**TERMS AND CONDITIONS:-**
1. Bid must submit in sealed envelope clearly marked "BID FOR THE PURCHASE ZACHARIA HANS POPPE AND Z. H POPPE LTD PROPERTIES, including full address of the bidder.
2. The successful Bidder shall be required to deposit 25% of the bid price within 7 days from the date of the award and balance 75% of the bid price within 30 days from the date of the award or within such other time as we may prescribe; failure of which the offer shall be revoked forthwith and the 25% down payment shall be forfeited and the next highest bidder who meets the conditions may be awarded, or cancel the sale process altogether.
3. Bids must be submitted and shall be opened on the date and address described in the table above. Bidders are invited to attend opening ceremony event if they so wish.
4. The property is being sold on "AS THEY ARE", the Bank and us shall have no further liability after the sale.
5. The interested parties will be allowed to inspect the property by prior appointment.
6. All the information contained in this advertisement is free from liability.
7. The successful bidder or otherwise shall be notified within a maximum of seven (7) working days after bid opening: either to his physical address or his email address, which shall be sufficient communication.
8. The bank and we shall not be bound to accept the highest bid or any bid at all or reject any or all the bids without having to assign any reasons.
9. All costs regarding transfer of ownership shall be borne by the successful bidder.
10. All bids shall be addressed to the address below;

**For further information please contact: 0719206984 or 0716943424**
**Visit our office located at Mbezi Beach area**
**Contact us via Email: bilostarcompany@gmail.com;**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wafuasi wanne wa Trump wataka kuipindua serikali

**WASHINGTON,** Marekani

WANACHAMA wanne wa kundi la itikadi kali la mrengo wa kulia nchini Marekani 'Oath Keepers' wamepatikana na hatia ya njama ya kuipindua serikali kwa kuhusika kwao katika shambulizi la Januari 6, 2021 dhidi ya Bunge la Marekani, lililofanywa na wafuasi wa Rais wa zamani, Donald Trump (pichani).

**Wanne hao pia walipatikana na hatia ya kulizuia Bunge kuidhinisha uchaguzi wa rais wa 2020.**

Uamuzi huo unaashiria mwisho wa kesi ya pili kubwa ya uchochezi dhidi ya wanachama wa kundi hilo, ambao walikuwa miongoni mwa mamia walioshambulia Bunge la Marekani katika jaribio ambalo halikufanikiwa la kulizuia Bunge kuidhinisha ushindi wa Joe Biden dhidi ya Trump, katika uchaguzi wa rais wa 2020.



Wajumbe 12 wa jopo la wasaidizi wa mahakama wamewapata wanachama wa Oath Keepers David Moerschel, Joseph Hackett, Roberto Minuta na Edward Vallejo na hatia ya njama ya kuipindua serikali.

Wanne hao pia walipatikana na hatia ya kulizuia Bunge kuidhinisha uchaguzi wa rais wa 2020 na mashtaka mengine mawili ya njama yanayohusiana na shambulio la Bunge. **VOA**



Maofisa wa polisi wakifungua mlango wa gari nje ya eneo la Torrance, California, sehemu ambayo inatajwa kuwa mshukiwa wa mauaji ya watu 10 amejificha. **PICHA: AFP**

## Wafuasi wasifu utawala wa Rais Tshisekedi

**KINSHASA,** DRS

WAFUASI wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Félix Tshisekedi (pichani chini), wamesifu tathmini ya utawala wa rais huyo wakati akitimiza miaka minne madarakani tangu alipochukua hatamu 2019.

Wafuasi hao walijivunia tathmini ya Rais Tshisekedi ambayo wanaielezea kuwa chanya kwa kiasi kikubwa, wakiamini kwamba anastahili muhula wa pili, huku upinzani na mashirika ya kiraia wakimzungumzia Tshisekedi kushindwa kwenye ngazi zote.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha PPRD, chama cha Rais wa zamani Joseph Kabila, alisema Rais Tshisekedi ameshindwa kabisa kwani inaonekana wazi kuwa DRC inarudi nyuma kila siku kutokana na uongozi mbovu.

"Kwenye ngazi ya kisiasa kwa mfano, tume ya uchaguzi haijakuwapo wakati tayari tuko Januari tukianza mwaka wa uchaguzi. Kuhusu usalama hata tusizungumzie kwani idadi kubwa ya wananchi wanatawaliwa na majeshi ya kigeni na hatuoni mpango wa serikali ili kuwaondoa kabla ya uchaguzi," alisema.

Baadhi ya mashirika ya kiraia pia yanaunga mkono kauli hiyo, huku wakimshutumu Rais huyo kwa ahadi nyingi zisizotimizwa, ikiwamo kutekwa nyara mchakato wa uchaguzi pamoja na hali ya usalama kuendelea kuzorota mashariki mwa nchi hiyo.

"Rais wa DRC aliendelea kuwaahidi Wakongo kama ataboresha hali ya maisha yao, ila baada ya miaka minne hatujaona hali hiyo kuboreshwa. Tulichokitambua ni kwamba matendo ya rais pamoja na serikali yake havijaambatana na ahadi hizo. Tuliona pia akichukua hatua kiholela ambazo ziliharibu hali ya usalama," alisema.

Chama cha UDPS cha Rais Félix Tshisekedi pamoja na muungano wa vyama vinavyomuunga mkono kwa ujumla, vinajivunia mafanikio yake vikiamini kwamba tathmini yake inakidhi mahitaji mengi ya Wakongo, kama alivyoeleza Ntumba Tshabola Bintu, mbunge wa UDPS. **DW**



## Saba wauawa katika mashambulio California

**WASHINGTON,** Marekani

WATU saba wameuawa katika matukio mawili ya kupigwa risasi katika shamba la uyoga na kwenye kampuni ya lori katika jamii ya pwani kusini mwa San Francisco.

Hayo yalibainishwa jana na vyanzo rasmi, na kwamba mshukiwa mwenye umri wa miaka 67, Zhao Chunli, amekamatwa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wasimamizi wa Kaunti ya San Mateo Dave Pine, kulikuwa na mfanyakazi mwenye hasira eneo tukio lilipotokea.

Pia alisema watu wanne wameuawa katika shamba hilo na wengine watatu katika kampuni ya lori nje kidogo ya Half Moon Bay, mji ulio umbali wa maili 30 kusini mwa San Francisco, katika jimbo la California.

"Hakuna tishio linaloendelea kwa jamii kwa wakati huu," ofisi ya mkuu wa kaunti hiyo ilisema.

Matukio hayo yanafuatia vifo vya watu 11 Jumamosi kwenye ukumbi wa densi katika jimbo hilo la California. **RFI**

## Ufisadi waikumba Ukraine, Ulaya ikizozana kuitumia vifaru

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, amesema anafanya mabadiliko ya maofisa wake wa ngazi ya juu na chini serikalini, kutokana na madai makubwa ya ufisadi kuibuka nchini humo tangu Russia iivamie nchi hiyo Februari 2022.

Inaelezwa kuwa polisi wa kukabiliana na ufisadi nchini Ukraine walisema kwamba wanamshikilia naibu waziri wa miundo msingi kwa madai ya kupokea rushwa ya dola laki nne katika uagizaji wa jenereta kutoka nje ya nchi mwezi Septemba 2022.

Utafiti mmoja wa gazeti pia uliituhumu wizara ya ulinzi kwa kulipa fedha kupita kiasi kwa ajili ya chakula cha wanajeshi na kwamba Ukraine ina historia ndefu ya ufisadi na utawala usio thabiti.

Katika ujumbe wake wa video anaoutoa kila usiku, Zelenskiy jana alisema "Tayari kuna maamuzi binafsi, mengine nitayatoa leo 'jana, mengine kesho 'leo' kuhusiana na maofisa wa ngazi tofauti katika wizara na serikali kuu na hata pia katika serikali za majimbo na idara ya polisi".

Vyombo kadhaa vya habari nchini Ukraine vimeripoti kwamba huenda mawaziri na maofisa waandamizi serikalini huenda wakaachishwa kazi mara moja.

Sakata hilo la ufisadi linatajwa huenda litasababisha nchi za Magharibi kufikiria mara mbili kuhusiana na kuipelekea Ukraine misaada, wakati kukiwa na vuta ni kuvute miongoni mwa mataifa ya Ulaya kuhusiana na kupeleka nchini humo, vifaru vya kivita kutoka Ujerumani.

Ukraine inasema inavihitaji vifaru hivyo chapa Leopard 2 ili kukabiliana na jeshi la Russia na kuyarudisha katika himaya yake maeneo yaliyotekwa.

Ujerumani ambayo ni lazima itoe ridhaa ya vifaru hivyo kupelekwa Ukraine, inaonekana kusuasua kwa hofu ya kuichokoza Russia na kuvizidisha vita hivyo. **DW**

HABARI MICHEZO

# RAGE AZISHTUKIA TIMU TPL

**Na Adam Fungamwango**

KIONGOZI wa zamani wa Simba na soka la Tanzania, Ismail Aden Rage, amesema timu nyingi za soka nchini zimekuwa zikitumia muda mwingi kuuchezea mpira na kupigiana pasi nyingi kuliko kushambulia kwa ajili ya kutafuta mabao.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, Rage ameonyesha kushangazwa na hali hiyo, akisema kwa sasa timu nyingi zimeonekana kusaka zaidi pointi nyingi za umiliki wa mpira badala ya kutafuta mabao.**

Aliongea maneno hayo muda mfupi tu baada ya kutoka kutazama mechi kati ya Yanga dhidi ya Ruvu Shooting.

Kwenye mechi hiyo Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Mpoki Mwakinyuke ambaye alijifunga mwenyewe.

Rage alisema kwenye mechi hiyo, Yanga ingeweza kupata mabao mengi zaidi, lakini walitumia muda mrefu kuremba mpira, akishangaa kuwa siku hizi imekuwa ni tabia ya timu nyingi za Ligi Kuu.

"Wamejitafutia wenyewe, wala Yanga isingeshinda bao moja, wametumia muda mwingi kuuchezea mpira badala ya kushambulia moja kwa moja. Kama wangeshambulia moja kwa moja nadhani wangepata na hiyo nimeona ni udhaifu wa timu nyingi kwa sasa hapa Tanzania, wamekuwa wakiiga mpira wa kupasiana sana mpira kwa pasi ambazo hazina sababu za msingi badala ya kufanya mashambulizi, ili wapate pointi nyingi kwenye kuumiliki mpira. Utaona timu inakwenda mbele halafu ghafla utaona wanarudisha tena mpira nyuma, sasa huo siyo mpango mzuri hata kidogo kama timu inataka ushindi," alisema Rage ambaye amewahi kuongoza soka kwenye chama cha soka nchini (FAT), ambapo kwa sasa ni Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

Alichokisema Rage ndicho ambacho kinaonekana kutaka kubadilishwa na Kocha Mkuu wa sasa wa Simba, Roberto Oliveira, ambaye anaonekana kutaka kikosi chake kucheza soka la kushambulia moja kwa moja na kwa kasi, badala ya kukaa na mpira muda mrefu wachezaji wake wakipasiana na kupiga pasi nyingi za nyuma.



Mchezaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto), akiwatoka mabeki wa Ruvu Shooting wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baina ya timu hizo uliopigwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam. Yanga ilishinda 1-0. **PICHA: YANGA**

# *Singida Big Stars yaiwashia taa Azam*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 ilioupata juzi kwenye Uwanja wa Liti, Singida dhidi ya Azam FC, timu ya Singida Big Stars ni kama sasa inaitaka kwa udi na uvumba nafasi ya tatu ambayo kwa muda mrefu imekaliwa na Wanalambalamba hao.

Bao la Bruno Gomes, akifikisha idadi ya mabao manane kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu, liliifanya timu hiyo kufikisha pointi 43 sawa na Azam FC, ikiwa imedhidiwa mabao ya kufunga.

Azam FC iko juu kwa mabao 36 ya kufunga, huku Singida Big Stars ikiwa na mabao 24, lakini zote zikiwa zimecheza mechi 21.

Matokeo hayo hayakuwa mazuri kwa Azam FC, kwani yanaiweka kwenye hali ngumu kuipata nafasi ya tatu ambayo ni ya mwisho kwa zile zinazoipatia Tanzania mwakilishi kwenye michuano ya kimataifa.

"Nafikiri tumecheza mechi nzuri mno, na hiki ndicho ambacho makosa tunakitaka, niliwaambia wachezaji wangu kuwa tunakwenda kucheza kwa kushambulia, ingawa tumepata bao moja lakini nimefurahi," alisema Kocha Mkuu wa Singida Big Stars Hans van der Pluijm.

Nahodha wa timu hiyo Deus Kaseke alisema mechi ilikuwa na upinzani mkubwa, lakini wanashukuru kwa kupata ushindi.

"Mechi ilikuwa na upinzani mkubwa, tulitofautiana pointi tatu, tumefuata maelezo ya mwalimu tumepata matokeo," alisema.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Aggrey Morris, aliwapongeza wapinzani wao, akisema wao walifanya makosa yaliyosababisha kuadhibiwa.

"Tumefanya makosa, tunakwenda kujipanga na mechi inayokuja, timu kama haijacheza vizuri inafungwa, ila hawa ni binadamu, tunasahau tunaangalia ya mbele," alisema nahodha huyo wa zamani wa timu hiyo.

Bruce Kangwa, mchezaji wa Azam FC, alisema hayo ndiyo matokeo ya mchezaji wa mpira wa miguu, walijitahidi kila njia lakini imeshindikana, wakafungwa.

## Uchaguzi Taswa wasogezwa mbele

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Michezo la Taifa Tanzania (BMT) limeusogeza mbele uchaguzi wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (Taswa) uliokuwa ufanyike Januari 28, mwaka huu na badala yake umepangwa kufanyika Februari 2 kutokana na mwitikio mdogo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Mkuu wa kitengo cha uhusiano na mawasiliano BMT, Najaha Bakari, alisema wameamua kuusogeza mbele uchaguzi huo baada ya kuona mpaka sasa wamejitokeza waandishi 8 kuchukua fomu hizo.

"Baraza linasikitika kuona mpaka sasa waandishi wa habari za michezo Tanzania wana suasua kuchukua fomu za uongozi ndani ya chama hicho tunasisitiza waje kuchukua fomu ili waonyeshe mfano kwenye vyama vingine, alisema Bakari.

Kaimu huyo alisema waandishi wanapaswa kuchukua fomu kwani lengo ni kuona chama hicho kinasimamia utawala bora.

Alisema sifa ya mgombea anatakiwa awe na cheti cha taaluma ya uandishi wa habari kutoka kwenye chuo kinachotambulika nchini.

Wakati huo huo alitangaza uchaguzi wa Chama cha Tenesi Tanzania( TTA) ambao utafanyika Februari 25 mwaka huu.

Alisema nafasi ambazo zinawaniwa katika chama hicho ni Rais, Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi pamoja wajumbe.

## Fainali BSS Februari 4

**Na Mwandishi Wetu**

FAINALI ya tamasha la kusaka vipaji Tanzania, Bongo Star Search (BSS) itafanyika Februari 4, mwaka huu katika ukumbi wa The Super Dome Masaki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Kampuni ya Benchmach ambayo ndio waandaaji wa shindano hilo, Rita Paulsen amesema msimu huu umekuwa wa tofauti na misimu yote kwa kuwa wamechukuwa washiriki wa miaka yote wa kumi bora.

Alisema mshindi wa kwanza atapa Sh. milioni 20, mshindi wa pili milioni 3 na watatu milioni 1.

"Wamewekwa pamoja washindi waliofika kumi bora na kutengeneza mastaa wapya kwenye msimu huu wa kumi na tatu kwa malengo ya kuwapatia mashabiki wa kipindi chetu radha mpya tofauti na vipindi vingine."

"Kuwapatia wasanii wachanga fursa ya kuonekana zaidi na jamii yetu, kuwawezesha kuwa mastaa kwa nyimbo zao wenyewe hadi sasa waliofika 8 bora wamepata nafasi ya kurekodi na kufanya video za nyimbo zao wenyewe mpya."

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAKOMAA NA ENZO

KLABU ya Chelsea haijakata tamaa ya kumsajili kiungo wa kati wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez, mwenye umri wa miaka 22 katika dirisha la uhamisho la Januari baada ya ofa yao ya mwanzoni mwa mwezi huu kukataliwa. ***(Record)***

### FIRMINO NA MKATABA

LIVERPOOL pia wapo kwenye mazungumzo na Roberto Firmino mwenye miaka 31 juu ya mkataba wa muda mfupi. ***(Fabrizio Romano)***

### CAMAVINGA AWINDWA

KLABU ya Arsenal inajipanga kumvuta kwa mkopo kiungo wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye miaka 20 kama sehemu ya kuimarisha kikosi chao ambacho kinaongoza katika mbio za kuwania ubingwa wa EPL.***(Evening Standard)***

### REUS ATAKIWA

KLABU ya Manchester United inapiga hesabu za kumsajili kwa mkopo kiungo wa klabu ya Borussia Dortmund, Marco Reus mwenye miaka 33 baada ya kocha, Erik ten Hag kukutana na wakala wa mchezaji huyo. ***(Caught Offside)***

### TUCHEL HANA MPANGO

KOCHA wa Ujerumani, Thomas Tuchel hatazamii kuchukua usukani wa kuifunza klabu ya Tottenham Hotspur endapo nafasi hiyo itajitokeza na badala yake ana mipango ya kujiunga na Barcelona au Real Madrid. ***(Florian Plettenber)***

### JUDE ATAKIWA KUKATAA

KOCHA wa Borussia Dortmund, Edin Terzic amemtaka Jude Bellingham mwenye miaka 19, "kuvunja minong'ono" na kukataa ofa za usajili kutoka Real Madrid na Liverpool. ***(Mirror)***

### LEICESTER YATUMA OFA

KLABU ya Leicester City imetuma ofa mpya kwa klabu ya Stoke City ili kumnasa beki raia wa Australia, Harry Souttar mwenye miaka 24, baada ya dau la awali la pauni milioni 10 kukataliwa. ***(Mail)***

### CHAMBERS KUONDOLEWA

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anatarajiwa kumwondoa kwenye kikosi chake beki Calum Chambers aondoke katika harakati za kukifumua kikosi cha Villa - na hii itakuwa mara ya pili kwa kocha huyo kumuacha beki huyo mwenye miaka 28 - mara ya kwanza alimwacha kwa sababu kama za sasa walipokuwa Arsenal. ***(Mirror)***


### FRANCA AWANIWA

KLABU ya Newcastle United inaendelea na mazungumzo na klabu ya Flamengo ili kuafikiana juu ya makubaliano ya kumsajili mshambuliaji kinda wa Brazil Matheus Franca mwenye miaka 18. (90min)

### MAN WALIMTAKA GRIEZMANN

KLABU ya Manchester United ilifanya mazungumzo na mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ufaransa, Antoine Griezmann, 31 msimu uliopita wa joto kabla ya kupata uhamisho wa kudumu kwenye kikosi cha Diego Simeone. ***(Sky Sports)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANE: TUNAMLIPA CONTE KWA USHINDI

●●● Ni baada ya kuwafumua Fulham na kusogea kwenye nne bora ya Ligi Kuu England...

**LONDON,** England

HARRY Kane anataka kumlipa Antonio Conte kwa ushindi baada ya kufunga kwenye ushindi wa 1-0 dhidi ya Fulham.

**Nahodha huyo wa England aliifikia rekodi ya ufungaji wa muda wote ya Jimmy Greaves ya mabao 266 kwa Spurs baada ya kufunga bao la pekee na la ushindi pale kwenye uwanja wa Craven Cottage.**

Ushindi uliwafanya vijana hao wa Conte kubakiza pointi tatu kufika kwenye nne bora ya Ligi Kuu ya England, ingawa wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Baada ya kichapo cha 2-0 kutoka kwa Arsenal na kupoteza 4-2 kutoka kwa Manchester City, Kane alifichua kuwa wachezaji wa Spurs walifanya mazungumzo na Conte na yakazaa matunda jijini London siku ya Jumatatu.

Nyota huyo wa Tottenham aliambia Sky Sports: "Conte amepitia wakati mgumu nje ya soka na maisha yake binafsi. Kuwa sehemu ya timu si wachezaji pekee, ni kocha, wafanyakazi na kuwa pamoja kwa ajili ya kila mmoja.

"Tunataka kushinda kila mchezo kwa ajili yake. Anaweka shauku kubwa katika kila kipindi cha mazoezi. Na tunataka kumlipa kwa ushindi.

"Tulikuwa na mkutano mzuri kati yetu na kocha katika wiki ili tu kuzungumza na kurejea. Tutaendelea kupambana.

"Yeye ni kocha mwenye mapenzi na inabidi tuendelee kumfanyia kazi kwa bidii."

Spurs kwa kiasi kikubwa walikuwa fiti kipindi cha kwanza dhidi ya Fulham, ambao walikosa nafasi ya kuiruka Tottenham hadi nafasi ya tano.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,069,8

JACKPOT
MECHI WIKI HII

TAREHE: 25,26 NA 27 JANUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/01/23 | 20:30 | Mainz vs Borussia Dortmund | 2.83 | 3.52 | 2.26 |
| 02. 25/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Heerenveen | 2.82 | 3.36 | 2.34 |
| 03. 25/01/23 | 22:30 | SC Freiburg vs Eintracht Frankfurt | 2.46 | 3.42 | 2.63 |
| 04. 25/01/23 | 22:30 | Augsburg vs Monchengladbach | 2.96 | 3.40 | 2.23 |
| 05. 25/01/23 | 22:30 | Werder Bremen vs Union Berlin | 2.73 | 3.13 | 2.53 |
| 06. 26/01/23 | 00:00 | Osasuna vs Sevilla FC | 2.32 | 3.08 | 3.13 |
| 07. 26/01/23 | 02:30 | Santo Andre SP vs Botafogo SP | 2.63 | 2.94 | 2.63 |
| 08. 26/01/23 | 10:45 | Melbourne Victory vs Sydney FC | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 26/01/23 | 14:00 | Aizawl FC vs Mohammedan SC | 2.81 | 3.22 | 2.31 |
| 10. 26/01/23 | 20:45 | Groningen vs Cambuur | 2.19 | 3.37 | 3.07 |
| 11. 26/01/23 | 22:00 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.08 | 2.63 |
| 12. 27/01/23 | 06:00 | Club Atlas vs Santos Laguna | 2.66 | 3.30 | 2.53 |
| 13. 27/01/23 | 11:45 | Newcastle Jets vs Brisbane Roar | 2.76 | 3.23 | 2.48 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GIROUD ANAPANGA KUENDELEA NA UFARANSA NA MILAN

**MILAN,** Italia

OLIVIER Giroud anapanga kusaini mkataba mpya na AC Milan na hayuko tayari kuahirisha maisha yake ya kimataifa na Ufaransa pia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 mkataba wake na kikosi cha Serie A ukimalizika Juni na amekabiliwa na maswali kuhusu mustakabali wake wa kimataifa kutokana na kushindwa kwa Les Bleus katika fainali ya Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Argentina.

Ufaransa tayari imemuona nahodha Hugo Lloris akitundika daruga kuitumikia timu ya taifa, huku Karim Benzema pia akistaafu.

Hata hivyo, Giroud, ambaye alikuwa mfungaji bora wa muda wote wa Ufaransa wakati wa michuano hiyo, hana mpango wa kuiga mfano huo.

"Kwa sasa ninaendelea na timu ya taifa. Nilishangazwa na ukweli kwamba Hugo ameamua kuondoka, uhusiano wetu ni maalum," aliiambia Canal Football Club.

"Lolote linaweza kutokea, sijajiondoa kwenye jukwaa la kimataifa na kwa sababu hii bado ninaweza kuitwa.

"Lazima nielewe ikiwa bado nataka kuvaa jezi ya bluu, ambayo ina maana kubwa kwangu, nataka kuchukua muda kabla ya kuamua."



## 'Arteta amebadilisha kila kitu'

**LONDON,** England

NAHODHA wa zamani wa Arsenal, Cesc Fabregas anaamini kuwa klabu hiyo imebadilika kila kitu chini ya kocha, Mikel Arteta.

Eddie Nketiah alifunga dakika za lala salama dhidi ya Manchester United kwenye Uwanja wa Emirates Jumapili na kuwapa Arsenal ushindi wa 3-2, na kuendeleza uongozi wa pointi tano dhidi ya Manchester City kileleni mwa Ligi Kuu ya England.

Arsenal wamefurahia ufufuo wa ajabu chini ya Arteta, ambaye amefanya mabadiliko ya jumla katika klabu hiyo.

Fabregas amefichua kwamba safari ya hivi majuzi ya London ilionyesha "kila kitu kilikuwa kimebadilika" tangu enzi zake Arsenal.

"Nilikuwa na bahati ya kuwa kwenye uwanja wa mazoezi hivi majuzi na nilihisi kama sikuwahi kufika hapo awali kwa sababu kila kitu kilikuwa kimebadilika sana,"alisema akiambia Sky Sports.

"Meneja wa uwanja wa mazoezi aliniambia kuwa asilimia 95 ya mabadiliko yalikuwa ya Mikel.

"Amebadilisha mtazamo wa klabu, jumbe nyingi chanya kwenye uwanja wa mazoezi, vifaa vikubwa zaidi, vifaa bora, viwanja ni bora.

"Katika kiingilio wana alama ya Ligi Kuu tupu. Arteta anataka kutuma ujumbe kwamba: 'jamani, tunahitaji kuweka kazi ndani'.

## HABARI MICHEZO


861,169/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/01/23 | 18:00 | Hull City vs Queens Park Rangers | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 02. 28/01/23 | 18:00 | Blackburn Rovers vs Birmingham City | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 03. 28/01/23 | 23:00 | Getafe CF vs Real Betis Seville | 2.95 | 2.95 | 2.55 |
| 04. 29/01/23 | 14:15 | FC Twente Enschede vs Feyenoord Rotterdam | 2.75 | 3.45 | 2.40 |
| 05. 29/01/23 | 15:00 | OGC Nice vs Lille OSC | 2.95 | 3.30 | 2.35 |
| 06. 29/01/23 | 15:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 07. 29/01/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Valencia CF | 3.10 | 3.25 | 2.28 |
| 08. 29/01/23 | 16:30 | Brighton & Hove Albion vs Liverpool FC | 2.65 | 3.50 | 2.45 |
| 09. 29/01/23 | 17:00 | AJ Auxerre vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 29/01/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs FC Nantes | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 11. 29/01/23 | 17:30 | Schalke 04 vs 1. FC Cologne | 2.95 | 3.40 | 2.29 |
| 12. 29/01/23 | 18:00 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 3.05 | 3.30 | 2.29 |
| 13. 29/01/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Atletico Madrid | 3.20 | 3.20 | 2.26 |
| 14. 29/01/23 | 18:45 | SC Cambuur vs Fortuna Sittard | 2.75 | 3.35 | 2.45 |
| 15. 29/01/23 | 19:30 | Bayer Leverkusen vs Borussia Dortmund | 2.46 | 3.50 | 2.65 |
| 16. 29/01/23 | 20:30 | RC Celta de Vigo vs Athletic Bilbao | 2.85 | 3.00 | 2.55 |
| 17. 29/01/23 | 21:00 | Boavista Porto vs Portimonense SC | 2.27 | 3.20 | 3.15 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 25/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2767 | Turan Tovuz vs Karabakh | 16.58 | 5.39 | 1.17 |
| 13:00 | 3629 | Kenya Commercial Bank vs Posta Rangers | 1.74 | 3.10 | 4.96 |
| 13:27 | 3932 | Ural Yekaterinburg vs Botev Plovdiv | 2.20 | 3.47 | 2.80 |
| 13:30 | 1056 | Chador Malu Yazd vs Khosheh Talaei | 2.32 | 2.54 | 3.63 |
| 13:30 | 3083 | Chooka Talesh FC vs Arman Gohar Sirjan | 2.80 | 2.85 | 2.56 |
| 13:30 | 3710 | Kheybar Khorramabad FC vs Fajr Sepasi | 2.27 | 2.64 | 3.57 |
| 13:30 | 5132 | Saipa Karadj vs Shahrdari Astara | 1.73 | 2.90 | 5.60 |
| 14:00 | 5051 | Nairobi City Stars FC vs Wazito | 2.02 | 3.05 | 3.62 |
| 14:30 | 4541 | Rans Nusantara vs Bali Utd Pusam | 3.78 | 3.31 | 1.87 |
| 15:00 | 2519 | Nzoia United vs Vihiga Bullets FC | 1.50 | 4.00 | 5.40 |
| 15:00 | 3531 | Kariobangi Sharks vs Bandari | 2.66 | 2.87 | 2.66 |
| 15:00 | 3925 | AFC Leopards vs Kenya Police | 2.76 | 2.82 | 2.61 |
| 15:00 | 4474 | Bidco United vs Mathare United | 1.53 | 3.63 | 5.80 |
| 15:15 | 4659 | Tusker vs Ulinzi Stars | 1.96 | 2.90 | 4.09 |
| 15:30 | 2509 | Zira vs FK Sumgayit | 1.69 | 3.42 | 4.66 |
| 16:00 | 1542 | CS Sfaxien vs ES Sahel | 3.58 | 2.64 | 2.26 |
| 16:00 | 2103 | Esperance Tunis vs Stade Tunisien | 1.40 | 3.73 | 8.50 |
| 16:00 | 3333 | US Monastir vs ES Metlaoui | 1.42 | 3.42 | 9.74 |
| 16:00 | 4049 | AS Slimane vs Africain | 3.63 | 2.51 | 2.35 |
| 16:00 | 5044 | EO Sidi Bouzid vs Olympique de Beja | 2.53 | 2.54 | 3.20 |
| 16:00 | 5216 | ES Hammam Sousse vs Club A Bizertin | 2.42 | 2.53 | 3.43 |
| 16:00 | 5475 | US Tataouine vs CS Chebba | 2.19 | 2.74 | 3.57 |
| 18:00 | 1639 | FAR Rabat vs Ittihad Tanger | 1.37 | 4.03 | 8.06 |
| 18:00 | 2078 | Maghreb Tetouan vs Mouloudia Oujda | 2.20 | 2.86 | 3.38 |
| 18:30 | 1711 | Malkiya Club vs ISA Town | 2.15 | 3.31 | 3.00 |
| 18:30 | 1979 | Panserraikos vs AEK Athens | 8.89 | 4.96 | 1.27 |
| 18:30 | 4713 | Qalali vs Al-Tadamun Buri | 1.58 | 3.64 | 5.20 |
| 18:30 | 5502 | Busaiteen vs AL Ittihad Bhr | 1.84 | 3.52 | 3.67 |
| 20:30 | 2144 | Aris Salonica vs Olympiakos | 3.01 | 3.16 | 2.22 |
| 20:30 | 2377 | Mainz vs Borussia Dortmund | 2.77 | 3.57 | 2.28 |
| 20:45 | 1535 | GO Ahead Eagles vs AZ Alkmaar | 3.77 | 3.52 | 1.88 |
| 20:45 | 3057 | Vitesse Arnhem vs Twente | 3.43 | 3.38 | 2.03 |
| 21:00 | 1162 | BSG Chemie Leipzig vs Erfurt | 2.42 | 3.48 | 2.50 |
| 21:00 | 3868 | Berliner AK 07 vs Viktoria Berlin | 1.77 | 3.73 | 3.73 |
| 22:00 | 2580 | Fortuna Sittard vs Heerenveen | 2.91 | 3.26 | 2.33 |
| 22:30 | 1269 | SC Freiburg vs Eintracht Frankfurt | 2.47 | 3.41 | 2.62 |
| 22:30 | 2151 | Bayer Leverkusen vs VfL Bochum | 1.41 | 4.67 | 6.36 |
| 22:30 | 2521 | Halifax vs Scunthorpe | 1.72 | 3.71 | 4.29 |
| 22:30 | 4608 | Augsburg vs Monchengladbach | 2.92 | 3.46 | 2.23 |
| 22:30 | 5266 | Werder Bremen vs Union Berlin | 2.72 | 3.17 | 2.52 |
| 22:45 | 1868 | Chesham Utd vs Merthyr Town | 1.64 | 3.90 | 4.26 |
| 22:45 | 2812 | Porto vs Viseu | 1.13 | 7.28 | 12.48 |
| 22:45 | 5097 | Woking vs Torquay | 1.45 | 4.31 | 6.10 |
| 22:45 | 5439 | Eastleigh vs Barnet | 2.18 | 3.41 | 2.99 |
| 23:00 | 1274 | Utrecht vs SBV Excelsior | 1.38 | 4.78 | 6.77 |
| 23:00 | 4354 | Nottingham vs Manchester Utd | 4.66 | 3.57 | 1.72 |
| 23:00 | 5402 | Feyenoord vs NEC Nijmegen | 1.28 | 5.36 | 8.93 |
| 23:00 | 5618 | Barcelona vs Real Sociedad | 1.67 | 3.65 | 4.96 |
| 23:10 | 5672 | Union Magdalena SM vs Atletico Huila | 1.92 | 3.16 | 3.83 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KVZ HAIPOI LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ imesema moto waliouwasha katika mzunguko huu wa kwanza hawatarajii kuuzima mpaka wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

**KVZ juzi ilivuna pointi tatu na kuwa vinara wa Ligi kuu ya Zanzibar kwa kufikisha alama 37 baada ya kuwafunga Malindi FC waliokuwa wamefungana pointi.**

Akizungumza na gazeti hili kocha msaidizi wa timu hiyo, Ali Khalid alisema wanaendelea kuhakikisha wanavuna alama tatu kila wanaposhuka dimbani.

Alisema katika msimu wa dirisha dogo timu hiyo ilifanya usajili wa kuongeza wachezaji ambao watatimiza malengo yao ya ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Alisema licha ya kufanya vizuri michezo yote miwili ya mzunguko wa pili, lakini bado jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha wanaendelea kufanya vizuri.

"Tumefanya vizuri michezo miwili ya mwanzo na matarajio yetu tufanye vizuri zaidi ili lengo la kupata ubingwa litimie, tunacheza kwa mipango na wachezaji wanacheza kwa ari kubwa," alisema.

Aidha, alisema kuwa katika mchezo ujao dhidi ya KMKM utakaopigwa Januari 29, wamejipanga kucheza kwa mikakati ya kupata ushindi.



Vijana wanaolelewa katika kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Baleke aanza tambo

INATOKA UKURASA 24

matatu au manne, anaweza kuwa kwenye mbio hizo.

Wakati huo huo, klabu ya Simba imesisitiza kuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliveira, atarejea nchini Januari 31 kuendelea na majukumu yake tofauti na upotoshaji unaoendelea kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kuwa kocha huyo aliondoka usiku wa juzi kwenda nyumbani kwao nchini Brazil kushughulikia mambo binafsi na ya kifamilia.

"Ameondoka kwa ajili ya kushughulikia mambo binafsi na ya kifamilia na atarejea Janauari 31, muda mrefu alikuwa hapa Afrika na hakupata fursa ya kwenda kwao na imepatikana nafasi hii ya wiki moja ambayo haina mechi za Ligi Kuu, ameenda kwao kuweka mambo sawa, ataukosa mchezo mmoja tu dhidi ya Coastal Union hiyo hatuna shaka, Juma Mgunda atakiongoza kikosi na mwenzake Ouanane Sellami," alisema.

## *Fei Toto amuumiza kichwa Nabi*

INATOKA UKURASA 24

mfumo na kuona anaweza kucheza dakika ngapi, atacheza na nani na kwenye mfumo atacheza wapi pamoja na jinsi anavyosikilizana na wenzake uwanjani," alisema Nabi.

Alisema kuhusu kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo wa Ruvu Shooting haujaridhisha kwa sababu ya kujaribu mfumo mpya, kikubwa ni kupambana na kupata pointi tatu muhimu.

Kocha huyo alisema kujaribu mfumo mpya sio mara ya kwanza kuna wakati wachezaji hawapo ndio tunatafuta njia nyingine ya kupata matokeo mazuri ya idadi kubwa.

"Ruvu Shooting walicheza kwa kuzuia sana na kulazimika kutumia washambuliaji wawili kwa ajili ya kuwasukuma ili wafunguke na kufunga, walijitahidi kuzuia wasipate bao lakini tuliweza kupata ushindi huo wa bao 1-0 na kuondoka na pointi tatu," alisema Nabi.

Naye Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Mbwana Makata, alisema mchezo ulikuwa mgumu kwa sababu ya kila mmoja wao kuhitaji kupata matokeo mazuri pamoja na wao kufeli mipango yao.

"Mipango yetu ni kupata pointi moja hatukutaka kufunga katika mchezo huo, tuliwaheshimu sana Yanga lakini tulifanya makosa kipindi cha kwanza na kufungwa bao 1-0, kipindi cha pili tumecheza vizuri na kutoruhusu bao," alisema Makata.

Michezo
Jumatano Januari 25, 2023
Nipashe



Kane: Tunamlipa Conte kwa ushindi UKURASA 21

# Fei Toto amuumiza kichwa Nabi

●●● Asema inampa wakati mgumu wa kufanya mabadiliko ya mfumo...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema kutokuwapo kwa baadhi ya wachezaji akimtaja Feisal Salum 'Fei Toto' inampa wakati mgumu wa kufanya mabadiliko ya mfumo katika michezo yao.

**Yanga juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam, ambapo bao lilikuwa la kujifunga kupitia mchezaji Mpoki Mwakinyuke dakika ya 35.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema mchezo huo haukuwa rahisi kwa sababu ya mfumo mpya ambao wameujaribu kwa wachezaji wapya baada ya kukosekana kwa baadhi ya nyota muhimu akiwamo Fei Toto ambaye amegoma kurejea ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Alisema wanalazimika kutumia wachezaji wengine na wale wapya kubadili mfumo ambao utachukuwa muda mrefu kidogo kutengeneza muunganiko mzuri kama ilivyokuwa awali.

"Hii mechi haikuwa rahisi, tumepata muda mzuri wa kufanya mazoezi ikiwamo kujenga mwili, lakini kuna kazi kubwa kwa benchi la ufundi kubadilisha mfumo kwendana na wachezaji wapya kuingia katika mfumo na kupata matokeo yenye idadi kubwa ya mabao.

Kuna baadhi ya wachezaji ambao hawako katika kikosi, Fei Toto na Khalid Aucho tumewakosa na kuingia na mfumo mpya ambao tunaujaribu kidogo kidogo kuhakikisha timu inarejea katika ubora wao," alisema Nabi.

Alisema kuhusu muunganiko wa mshambuliaji wao mpya, Kennedy Musonda bado anahitaji muda wa kuzoeana na mfumo ndani ya kikosi cha timu hiyo.

"Musonda bado hajaingia mfumo na tunamwingiza taratibu, mechi ya kwanza na Ihefu FC alicheza dakika 30 na hii ya leo na Ruvu Shooting amecheza dakika 70 jumla ameitumikia dakika 90.

Kikubwa ni kumwingiza katika

INAENDELEA UKURASA 23



Fei Toto. PICHA: JUMANNE JUMA

# Baleke sasa aanza tambo za kufunga zaidi Simba

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mpya wa Simba, Jean Baleke, ameonyesha furaha kubwa kwa kucheza mechi ya kwanza akiwa na timu yake mpya na kuipatia bao la ushindi dhidi ya Dodoma Jiji Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, lakini akasisitiza kuwa yeye kufunga ni kitu cha kawaida sana kwenye klabu zote alizopitia kiasi cha kutungiwa nyimbo nyingi na mashabiki.

Akizungumza kwa mara ya kwanza tangu ajiunge na klabu hiyo kipindi cha dirisha dogo akitokea Nejmeh ya Lebanon, Baleke ambaye ni straika wa zamani wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo amesema bao alilofunga amelitoa maalum kwa wachezaji, makocha, viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba.

"Najisikia furaha kukutana na marafiki hapa, kuhusu kufunga bao, kwanza mimi kufunga ni kawaida yangu nimeshazoea, nasubiri mechi zinazokuja ili kuonyesha.

Nilipoona kocha amenipanga kwenye kikosi cha kwanza, nikajiweka tayari kufanya kitu ambacho kitaisaidia timu kupata ushindi kwa kufunga au kutoka pasi ya mwisho au msaada wowote wa kuwezesha timu kufanya vizuri na ushindi ule ulikuwa ni maalum kwa wachezaji, makocha, viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba, lakini haya yamepita ni muda wa kujiandaa kufikiria mechi ijayo.

Kuhusu mashabiki na wingi wake uwanjani nimeshazoea, tangu nilikotoka nimekuwa nikifunga sana na nimekuwa kipenzi cha mashabiki tangu nilikotoka na hata kuna nyimbo nyingi nimetungiwa na mashabiki wa klabu nilizotoka," alisema.

Alisema kwa sasa ana bao moja, hatojiingiza sana kwenye kinyang'anyiro cha ufungaji bora, lakini kwa mipango ya Mungu kama kuna mechi akitupia mabao

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >